*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00039 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Novemba 22 - 28, 2023 |


Uk. 24

Yanga yapata mfadhili Dubai



**Ni aibu mtoto kwenda shule kwa shinikizo la polisi** Uk.10


Uk.23

**Dalili 10 za saratani zisizotambulika kirahisi** Uk.15



**Mambo haya yanachangia wanaume kuchepuka** Uk.11

## UWEKEZAJI MKUBWA WA SAMIA :

# Muhimbili kutibu kiharusi kibingwa



**Na Godfrey Sanga**

UWEKEZAJI mkubwa uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), umeiwezesha hospitali hiyo kuanza kutoa tiba kwa wagonjwa wa kiharusi wa ndani ya saa 24. **Uk. 4**

## RC amtaka DC mguu kwa mguu


Uk.7

## Kiingereza kuanza darasa la kwanza 2024

**Na Mwandishi Wetu, Chalinze**

UTEKELEZAJI wa kufundisha somo la Kiingereza kuanzia darasa la kwanza kufuatia mabadiliko ya Mtaala wa Elimu ya Msingi 2023, utaanza rasmi Januari, mwakani. **Uk.4**

## Mchengerwa asimamisha kazi wakurugenzi wawili Uk. 2



## MNH, Kairuki wasaini makubaliano upatikanaji wa dawa Uk. 3



## Madereva bajaj watakiwa kufichua wahalifu Uk. 5

# Watu 23, 798,848 kupata huduma mawasiliano ya simu ya uhakika

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wananchi milioni 23 wanatarajiwa kupata huduma ya mawasiliano ya uhakika baada ya kukamilika kwa ujenzi wa minara 2,149.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasialino kwa Wote (UCSAF, Justina Mashiba, aliwaambia Wahariri na waandishi wa habari katika kikao kazi cha kuelezea mafanikio ya taasisi hiyo jijini Dar es Salaam jana.

Justina alisema pindi minara hiyo yote itakapokamilika kujengwa, takriban wananchi 23,798,848 watapata huduma bora ya mawasiliano.

Alifafanua kuwa UCSAF imeingia mikataba na watoa Huduma ya Mawasiliano (yaani kampuni za simu) kufikisha huduma ya mawasiliano katika kata 1,974 zenye vijiji 5,111 kwa kujenga jumla ya minara 2,149.



Afisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasialino kwa Wote (UCSAF, Justina Mashiba

Kwa mujibu wa Afisa Mtendaji huyo wa UCSAF, mpaka sasa, jumla ya kata 1,197 zenye vijiji 3,613 na wakazi takribani 14,572,644, wameshafikishiwa huduma ya mMawasiliano kutokana na kujengwa jumla ya minara 1,321 katika maeneo yao.

Justina aisema utekelezaji unaendelea katika kata 777 zenye minara 828, vijiji 1,498 na wakazi 9,226,204 kwa gharama (ruzuku) za utekelezaji wa Sh. bilioni 326. 326.

Kuhusu mradi wa Tanzania ya Kidigitali, Afisa Mtendaji Mkuu huyo wa UCSAF alisema jumla ya minara 758 itajengwa katika kata 713 na kwamba mikoa 26 itanufaika.

Aidha, wilaya 127 zitanufaika pindi mradi huo utakapokamilika ukinufaisha jumla ya wakazi milioni 8.5.

Kadhalika, Justina alisema mpaka sasa, jumla ya shule 1,120 zimefikishiwa vifaa vya Tehama kwa wastani wa shule kupewa kompyuta, printa moja na projekta moja.

Aliongeza kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2022/23, jumla ya shule 150 zilifikishiwa vifaa vya Tehama na kwamba bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa vifaa vya Tehama, ni Sh. 1,876,900,000.

# MNH yawasilisha kwa Balozi ombi la mafunzo

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Mohamed Janabi, amemuomba Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa, kutoa fursa kwa wataalamu wa Muhimbili kupata mafunzo mbalimbali ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

Alitoa ombi hilo baada ya Balozi Misawa kutembelea maeneo mbalimbali ya utoaji wa huduma ikiwemo Idara ya Magonjwa ya Dharura, Idara ya Radiolojia, Wodi Maalumu ya Uangalizi wa Watoto (PICU), Chumba cha Matibabu ya Dharura kwa Watoto pamoja na eneo linalojengwa jengo la wagonjwa wa kulipia.

Profesa Janabi alimweleza Balozi Misawa kwamba katika dunia ya sasa, mafunzo kwa wataalamu wa afya ni muhimu hasa katika uboreshaji wa huduma unaoenda sambamba na uanzishwaji wa huduma mpya za kibingwa na kibobezi kama Hospitali ya Taifa.

"MNH ina matawi mawili Upanga na Mloganzila, kuna watumishi 3,200 kwa pande zote mbili, watalaamu hawa wanahitaji kuendelea kupatiwa mafunzo yatakayowawezesha kuleta mapinduzi chanya ya utoaji huduma katika sekta ya afya hasa ukizingatia hospitali hii ni kubwa hapa nchini na inapokea wagonjwa wengi, hivyo, nitumie fursa hii kukuomba ikitokea nafasi za mafunzo, watumishi wa Muhimbili wapewe kipaumbele," alisema.

**MNH ina matawi mawili Upanga na Mloganzila, kuna watumishi 3,200 kwa pande zote mbili, watalaamu hawa wanahitaji kuendelea kupatiwa mafunzo...**



Mkurungenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Mohamed Janabi.

Kwa upande wake, Balozi Misawa alimpongeza Profesa Janabi kwa maboresho makubwa aliyoyafanya Muhimbili na kumuhakikishia kuwa yuko tayari kushirikiana na MNH katika kuendelea kuboresha utoaji wa huduma za afya.

Naye Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Dharura, Dk. Juma Mfinanga, alimweleza Balozi kwamba katika chumba cha huduma ya dharura cha watoto Muhimbili, kwa siku wanahudumia watoto kati ya 50 hadi 70 na kwamba wakifikishwa hufanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu kwa dharura.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala la Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa.

# Mchengerwa asimamisha kazi wakurugenzi wawili

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala la Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa, amewasimamisha kazi wakurugenzi watendaji wawili kuanzia Novemba 20, mwaka huu, ili kupisha uchunguzi kwa tuhuma za kusimamia miradi ya maendeleo katika halmashauri zao kwa nyakati tofauti.

Waliosimamishwa kazi ni Butamo Nuru Ndalahwa ambaye alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Kibaha mkoani Pwani na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara mkoani Morogoro.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na wizara hiyo jana, uamuzi wa kuwasimamisha kazi wakurugenzi hao imechukuliwa baada ya kupokea taarifa za awali ya timu ya iliyoundwa kuchunguza tuhuma zao za kushindwa kusimamia miradi ya maendeleo kwenye halmashauri zao kwa nyakati tofauti.

Aidha, Waziri Mchengerwa alisisitiza kuwa wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao kikamilifu ikiwa ni pamoja na kusimamia miradi ya maendeleo na kwamba hatua stahiki zitachukuliwa kwa ye yote atakayethibitika kwenda kinyume cha hapo.

# `Kipaumbele cha kibiashara kwa wanawake kuendelea'

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amesema wafanyabiashara na wajasiriamali wanawake, wameendelea kupewa kipaumbele kwenye majukwaa mbalimbali ya biashara na ujasiriamali ili kuhakikisha wanapata maendeleo na kukua kiuchumi kupitia shughuli hizo za biashara na ujasiriamali.

Alisema hayo kwenye Kongamano la Maandalizi na Masoko kwa Wanawake na Vijana Wajasiriamali lililofanyika jijini Dar es Salaam juzi.

Alisema Tanzania imeendelea kuandaa na kuratibu sera mbalimbali za kuwawezesha wanawake na vijana na kwamba wanafurahi na kupata maendeleo kupitia biashara hizo.

"Dar es Salaam tumekuwa na kipaumbele kikubwa kutoa fursa za biashara kwa wanawake ili kuwafanya kukua na kupata maendeleo kupitia biashara hizo na ujasiriamali," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Women Chamber of Commerce (TWCC), Mwajuma Hamza, alisema wanatoa mafunzo hayo kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wanawake katika majukwaa makubwa ili kuwawezesha kuyafikia na kupata mafanikio ili kukua kiuchumi na kupata maendeleo.

"Wanawake hawajalala, wanaendelea kuchangamkia fursa zaidi kwenye majukwaa mbalimbali ili kufikisha biashara zao ili zikue, sisi TWCC tunaendelea kuhamasisha zaidi hata wale wanawake wafanyabiashara wa mikoani ili na wao wachangamkie fursa hizi zilizopo," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila.



Rais wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapindui na Makamo Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Kamati ya UWT ya Uratibu wa Sherehe za miaka mitatu ya Uongozi wake walipofika kumshukuru Ikulu jijini Zanzibar jana. Picha Ikulu

# Vyuo vya Afya vyapewa mkakati



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Afya), Dk. Wilson Mahera, ameviagiza Vyuo vya Afya ambavyo havina kozi ya Shahada ya Udaktari wa Kinywa na Meno, kuianzisha ili kusaidia kuongeza upatikanaji wa watalaamu wengi zaidi hapa nchini.

Aliyasema hayo wakati akifungua Mkutano wa Madaktari wa Kinywa na Meno Tanzania uliofanyika kitaifa jijini Tanga juzi.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia upatikanaji wataalamu wengi ambao watasaidia katika utoaji wanakumbana na changamoto mbalimbali za afya ya kinywa na meno.

"Kupitia mkutano huu niagize vyuo vya afya nchini ambavyo havina kozi ya Shahada ya Udaktari wa Kinywa na Meno kuanzisha ili kusaidia kuongeza upatikanaji wa watalaamu hao hapa nchini," alisema.

Alisema kwa mfano, mwaka 2022 kitaifa kulikuwa na wagonjwa wa kinywa 747,858 waliooza meno 522,777 sawa na asilimia 68.9 ya wagonjwa wote wa kinywa na meno na waliokuwa na matatizo ya fizi ni 78,755.

Alisema kwa takwimu hizo tatizo la kuoza kwa meno bado ni kubwa hapa nchini bado na wana kazi kubwa ya kufanya wagonjwa 156,576 sawa na asilimia 30 walioza meno yalizibwa na wagonjwa 265,249 sawa 49.6 yaliny'olewa.

"Tatizo la meno yakikubana mtu ukiamka asubuhi yanang'olewa niwatake wataalamu mjikite zaidi kutibu na sio kuyang'oa kwa maana Serikali imewekeza miundombinu yote wezeshi kuhakikisha wananchi wanapatiwa tiba ya meno na sio kungoa jino," alisema.

Hata hivyo, alisema kwamba kuna maeneo ya huduma za kinywa na meno hazipatikani lakini bado wananchi wanatembelea umbali mrefu kufuata huduma hiyo jambo ambalo siyo sawa.

Aidha, aliagiza na kuwaelekeza waganga wakuu wa mikoa na halmashauri kuhakikisha vituo vya afya vya kimkakati na visivyo vya kimkakati vinaaza kutoa huduma ya matibabu ya kinywa na meno ili kuepusha wananchi

# MNH, Kairuki wasaini makubaliano upatikanaji wa dawa

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) na Kiwanda cha Dawa cha Kairuki KPTL, wamesaini Mkataba wa Makubaliano (MoU) kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa dawa Muhimbili Upanga na Mloganzila.

Mkataba huo uliosainiwa jana umeanisha maeneo mawili, moja ikiwa ni kuboresha upatikanaji wa dawa ambazo hazipatikani kwa urahisi kwenye soko ikiwemo zinazotumika katika upandikizaji wa viungo mbalimbali mwilini kama figo, kongosho pamoja na dawa zenye ujazo mdogo zinazotumika kwa watoto na wagonjwa wa saratani.

Eneo la pili ni kuwajengea uwezo wataalamu wa Muhimbili katika uzalishaji wa dawa na namna ya kuongeza kuzitumia dawa zinazozalishwa na kiwanda hicho.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, alisema hiyo ni hatua nzuri kuwepo kwa kiwanda cha dawa ambacho kinamilikiwa na wazawa na kukidhi viwango vinavyohitajika.

Pia, alifafanua kuwa Muhimbili ni hospitali kubwa kuliko zote nchini yenye vitanda 2,150 ambapo Upanga kuna vitanda 1,550 na Mloganzila kuna vitanda takribani 600, hivyo inawahudumia wagonjwa wengi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Dawa cha Kairuki, Dk. Muganyizi Kairuki alisema kiwanda hiko kimedhamiria kuzalisha bidhaa kulingana na mahitaji yaliyopo na kuhakikisha mkataba uliopo unakuwa na tija kwa hospitali.



Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi

# Kiharusi kutibiwa kibingwa



Na Godfrey Sanga

UWEKEZAJI mkubwa uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), umeiwezesha hospitali hiyo kuanza kutoa tiba kwa wagonjwa wa kiharusi wa ndani ya saa 24.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Profesa Mohamed Janabi, alisema ili kufanikisha matibabu hayo, tayari amekutana na uongozi wa Taasisi ya Weill Cornell Medicine ya Marekani kwa lengo la kuanzisha mpango maalumu wa matibabu ya wagonjwa wa kiharusi watakaofikishwa hospitalini hapo ndani ya saa 24.

Katika taarifa iliyotolewa jana kupitia akaunti ya mtandao wa kijamii wa Wizara ya Afya, Profesa Janabi alisema mpango huo utakuwa na manufaa makubwa kwa kuwa Muhimbili ina vifaa tiba vya kisasa vya kuhudumia wagonjwa wa kiharusi ikiwemo mtambo wa Angio-Suite ambao unatumika kufanya uchunguzi na matibabu ya kiharusi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Radiolojia, Dk. Fredrick Lyimo, alisema matibabu ya mgonjwa wa kiharusi, yanahusisha jopo la wataalamu wengi kuanzia pale anapopokelewa mpaka kupatiwa matibabu.

Dk. Lyimo aliongeza kuwa wataalamu hao watatembelea maeneo mbalimbali ambayo yanatumika kutoa huduma kwa wagonjwa wa kiharusi.

"Kwa sasa, watatembelea maeneo ya kutolea huduma kuangalia mtiririko mzima wa kuhudumia wagonjwa wa kiharusi kwa kuwa matibabu ya kiharusi yanahusisha wataalamu wengi ikiwemo madaktari wa mishipa ya fahamu, wataalamu wa kufanya vipimo vya radiolojia, kupiga picha na kusoma majibu," alisema.

Katika ziara hiyo, wataalamu hao walitembelea Idara ya Magonjwa ya Dharura na Idara ya Radiolojia ambapo wameangalia baadhi ya mashine za uchunguzi ikiwa ni pamoja na ANGIO-SUITE, MRI, X-RAY NA CT-SCAN.

Mpango huo utatoa ahueni kwa wagonjwa wa kiharusi hospitalini hapo ambapo taarifa zilizopo zinasema wagonjwa 30 kati ya 100 wa kiharusi wanaotibiwa hospitalini hapo, hufariki dunia kutokana na kuchelewa kufikishwa hospitali.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti Chama cha Wanasayansi wa Magonjwa ya Mishipa ya Fahamu Tanzania (TNA), Profesa William Matuja, aliyoitoa Oktoba 23, mwaka huu, wagonjwa wengi wanafikishwa hospitalini hapo wakiwa wamechelewa.

Alisema kutokana na ukubwa wa tatizo hilo wameanziasha mtandao wa kuelimisha na kutibu kiharusi kwa watumishi wa kada zote nchi nzima, jinsi ya kuhudumia mtu mwenye kiharusi kwa haraka.

Profesa Matuja alisema jamii haina uelewa wa kutosha namna ya kumhudumia mgonjwa wa kiharusi mara tatizo linapoanza.

"Kila sekunde anayocheleweshwa, ndiyo mgonjwa anakuwa kwenye hatari zaidi, wagonjwa wengi tunawapokea Muhimbili wakiwa wameshachelewa sana matibabu kwa wiki mbili mpaka mwezi," alisema.

Alisema: "Mtu anapata shida ya kiharusi badala awahishwe hospitali, anapelekwa huko kwa tiba za asili, mpaka analetwa hapa Muhimbili tayari kishachelewa."

Alisema tatizo la kiharusi kwa sasa linazidi kuwa kubwa nchini kiasi kamba hata vijana kwa sasa wanapata tatizo hilo.

Alitaja baadhi ya visababishi vya kiharusi kwa vijana na watoto kuwa ni mtindo wa maisha, tabia bwete, ulaji wa chumvi nyingi kwenye chakula na mafuta yaliyokithiri kwenye mishipa ya damu.

# Madereva bajaj watakiwa kufichua wahalifu

**Na Godfrey Sanga**

MADEREVA pikipiki za miguu mitatu (bajaj) mkoani Njombe, wametakiwa kuwafichua wahalifu waliopo katika maeneo wanayofanyia kazi ili kupunguza au kukomesha kabisa vitendo vya kihalifu katika mkoa huo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi wa Polisi ACP. Mahamoud Hassan Banga, alisema hayo kupitia mtandao wao wa kijamii wa Instagram baada ya mkutano wake na waandishi wa habari jana ambapo aliwataka kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za wahalifu wa matukio yanayohusu bajaj ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya wahalifu hao.

Hata hivyo, aliwataka madereva hao kufuata taratibu na Sheria za Usalama Barabarani, hususani, katika miteremko ili kupunguza ajali zisizokuwa za lazima.

Kwa upande wake, Mkuu wa Usalama Barabarani, Mrakibu wa Polisi Jane Warioba, aliwataka medereva hao kuzingatia alama za usalama barabarani na pia kuchukua tahadhari mapema kabla ya kushuka na kupanda katika miteremko kwa kufanya ukaguzi wa bajaj zao ikiwemo mifumo ya breki.

**Hata hivyo, aliwataka madereva hao kufuata taratibu na Sheria za Usalama...**

# Kamati yakoshwa maboresho ya miundombinu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, imepongeza jitahada zinazofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Yahya Rashid Abdallah, aliyeongozana na wajumbe wa kamati hiyo pamoja na wataalamu kutoka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ), alitoa pongezi hizo wakati walipofanya ziara ya mafunzo katika Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS).

Alisema Serikali imefanya kazi kubwa ya kuboresha miundombinu, hivyo Kamati ikaona ipo haja ya kujifunza na kubadilishana uzoefu baina ya Serikali ya Zanzibar na Tanzania Bara kwenye masuala ya uboreshaji wa miundombinu.

"Tumeona tuje tujifunze kutoka kwenu, tumeona kazi kubwa iliyofanyika chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, yale mazuri tutayachukua na kuyapeleka," alisema.

Awali, akitoa taarifa ya Wakala huo, Kaimu Meneja wa Tanroads, Dorothy Ntenga, alieleza kuwa Wakala unasimamia mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 11,966.38, mizani 76 za kupima uzito wa magari na madaraja 3, 139 katika barabara kuu na zile za mikoa.

Aidha, alisema Wakala huyo umekamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege saba na unaendelea na usimamizi wa utekelezaji wa ujenzi wa viwanja vingine tisa.

Akizungumza baada ya kutembelea mradi wa mabasi yaendayo haraka ya Awamu ya Tatu (BRT III), Mkurugenzi wa Mipango ya Miundombinu kutoka Tanroads, Efatha Mlav, alisema barabara zinazojengwa zinazingatia viwango, ambapo zinaweza kudumu kwa zaidi ya miaka 50.

Alisema kumekuwa na changamoto ya watu wengi kuharibu na kuingilia miundombinu ya barabara licha ya elimu kutolewa mara kwa mara.

Miongoni mwa miradi iliyotembelewa ni pamoja na barabara ya mabasi yaendayo haraka BRT awamu ya tatu pamoja na mradi wa daraja la Tanzanite.







# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

## Rushwa mpaka lini?

LICHA ya serikali kuendelea kupambana na rushwa katika maeneo mbalimbali, bado baadhi ya watumishi wa serikali wakiwemo askari polisi wameendelea kutengeneza mazingira ya rushwa. Ukiachana na wale wa usalama barabarani, bado kwenye vituo vya polisi kikiwemo kile cha Chanika, rushwa iko nje hata kama unakwenda kwa nia tu ya kumwekea dhamana ndugu yako.

Ni dhahiri, juhudi zinapaswa kuchukulia zaidi kwa watumishi wetu wa umma ili kuhakikisha rushwa ambayo bado ni adui wa haki na sumu ya maendeleo anakoma katika nchi yetu.

Ushauri wangu ni muhimu watu kuendelea kujitenga na rushwa. Pengine ni wakati mwafaka kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupabana na Rushwa (Takukuru) kuweka kambi au kuwa na ofisi katika maeneo yanayoaminika kuendesha vitendo vya rushwa kwa wingi.




MAONI YA MHARIRI

## Hongera Muhimbili kuzidi kuleta tiba za kibingwa

SASA hivi ni nadra kupita mwaka bila kusikia Hospitali yaTaifa ya Muhimbili (MNH) au taasisi nyingine kama Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) au Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na nyinginezo nchini kuanzisha tiba za kibingwa ambazo haikuwepo nchini.

Kuanzishwa kwa tiba hizi, umekuwa msaada mkubwa kwa Watanzania kwani ni huduma ambazo walikuwa wanalazimika kuzifuata nje ya nchi na kulipa gharama nyingi.

Tiba ya kibingwa ambayo kwa sasa unapata hapa nchini kwa gharama ya shilingi milioni tano, kwa mfano, njeulikuwa unaipata kwa Sh milioni 20 au zaidi mbali na gharama za usafiri na chakula.

Katika siku za karibuni tumesikia habari za kuanzishwa kwa tiba ya kutumia puto kupunguza unene na tiba ya upasuaji rekebishi ambayo inasaidia kupunguza au kuongeza maumbile kama ukubwa wa matiti na makalio, kupunguza tumbo au nyama kwenye mikono.

Hatua hii inazidi kuifanya Tanzania kuwa kituo cha utalii wa tiba kwani taarifa zinaonesha kwamba watu kutoka nchi jirani sasa wanakuja Tanzania kupata tiba hizi ambazo bado hazipo katika nchi zao.

Kutokana na uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, MNH jana imetangaza kwamba iko mbioni kutoa tiba kwa wagonjwa wa kiharusi wanaofikishwa hospitalini hapo ndani ya saa 24.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Profesa Mohamed Janabi, amesema kwamba ili kufanikisha matibabu hayo tayari amekutana na uongozi wa Taasisi ya Weill Cornell Medicine ya Marekani kwa lengo la kuanzisha mpango maalumu wa matibabu ya wagonjwa wa kiharusi watakaofikishwa hospitalini hapo ndani ya saa 24.

Tunapongeza hatua hiyo ya MNH na kwani mpango huo utatoa ahueni kubwa kwa wagonjwa wa kiharusi. Taarifa zilizopo zinaonesha kwamba wagonjwa 30 kati ya 100 wa kiharusi wanaotibiwa hospitalini hapo hufariki dunia kutokana na kuchelewa kufikishwa hospitalini na wengine kuishi katika mazingira magumu kutokana na baadhi ya viungo kushindwa kufanya kazi.

Tiba hiyo ikianza, wagonjwa watakaowahishwa ndani ya saa 24, asilimia kubwa watapona ugonjwa huo hatari.

Haya ni maendeleo makubwa na tunawahimiza MNH na taasisi nyingine za tiba nchini kuendelea kuleta tiba za kibingwa Tanzania.


### Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255787559090 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |





## Tuendelee na mapambano dhidi ya maadui watatu

BAADA ya Tanzania kupata Uhuru mwaka 1961 Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alitangaza vita dhidi ya maadui watatu; ujinga, umasikini na maradhi.

Kwa adui ujinga nchi ilihitaji kuelimisha watu wake kuondoka na elimu ya kikoloni kuwa ya kibaguzi, umaskini ulikuwa mkubwa na hivyo nchi ilikuwa na dhima ya kuwanyanyua wananchi wake kiuchumi lakini pia kulikuwa na tatizo la matibabu kutokana ni uduni wa miundombinu ya hospitali.

Tumepiga hatua kwa kiwango fulani katika mapambano dhidi ya maadui hao watatu lakini mengi zaidi yanapaswa kufanywa ili nchi yetu izidi kupaa kiuchumi na kupunguza umaskini.

Moja ya eneo ambalo serikali imefanya kazi kubwa ni elimu. Na leo nitajikita zaidi tika eneo hili na siku nyingine nikipata nafasi nitaangalia hayo mengine mawili yaliyobaki.

Kimsingi, elimu ni silaha muhimu sana ambayo mbali na kupambana na adui ujinga lakini ikitumika vizuri pia inasaidia katika kupambana na maadui wengine wawili waliobaki ambao bado wanatusumbua, umasikini na maradhi.

Ndiyo, kupitia elimu tunapata wataalamu kama walimu, madaktari, wahandisi, waandishi wa habari, marubani wa ndege na kadhalika. Lakini pia tunapata wafugaji na wakulima wa kisasa na hivyo kuondokana na kilimo cha mazoea.

Mbali na ujenzi wa shule takribani kila eneo la nchi yetu kwa maana ya shule za msingi, sekondari na hata vyuo, kumbukumbu zinaonesha kwamba serikali ya Rais Samia Suluhu inaendelea kufanya vizuri katika eneo hilo.

Hivi karibuni serikali ilivunja rekodi ya kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi aliyehitimu elimu ya sekondari anakwenda sekondari na hilo liliwezekana kutokana na kujenga madarasa ya kutosha.

Lakini serikali ya awamu ya sita pia imepanua wigo wa elimu bila ada kutoka chekeachea hadi kidato cha sita huku pia ikiongeza mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Pamoja na serikali kujenga shule nyingi bado kuna changamoto za hapa na pale zinazofanya ujinga uendelee kujichimbia katika nchi yetu. Zipo zinazoigusa serikali lakini nyingine zinatuhusu sisi wananchi wenyewe.

> **Lakini serikali ya awamu ya sita pia imepanua wigo wa elimu bila ada kutoka chekeachea...**

Baadhi ya changamoto zinazoigusa serikali ni kuhakikisha mazingira ya kusomea yanakuwa mazuri zaidi kama vile ujenzi wa mabweni kwenye shule za kata ili kunusuru watoto wa kike na vishawishi vya wanaume wapumbavu, kuajiri walimu wa kutosha katika kila shule na kupeleka vifaa vya kutosha katika shule kama vitabu vya kutosha, maabara, kompyuta na kadhalika.

Lakini kuna tatizo kwa wazazi kwani bado wapo ambao hawana mwamko wa elimu.

Inashangaza kusikia kwamba mzazi anamshauri mwanae kujifelisha darasani ili aolewe au akafanye biashara badala ya kuhimiza mtoto asome. Inasikitisha pia kugundua kwamba inafikia wakati serikali inaingilia kati kikamata wazazi kwa kushindwa kupeleka watoto wao shule licha ya serikali kutoia elimu bila ada.

Kama nilivyokwishadokeza, elimu ni silaha muhimu ambayo kama itatumiwa vizuri inaweza kutokomeza kabisa hawa maadui watatu.

# RC amtaka DC mguu kwa mguu kutatua changamoto

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ameitaka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilala, kushughulikia 'mguu kwa mguu' changamoto ya ubovu wa barabara za Kata ya Msongola iliyopo ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam mara baada ya mvua kupungua.

Alitoa maagizo hayo jana katika ziara yake ya kukagua maeneo ya miradi ya kiserikali inayoendelea kujengwa katika Kata za Msongola, Chanika na Zingiziwa ikiwemo ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Kata ya Msongola na ujenzi wa Zahanati ya Nzasa.

"Nimejionea changamoto za barabara na kwa sasa hazipitiki, hivyo basi, naelekeza ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilala, mvua zikipungua ni kuangalia mguu kwa mguu athari zilizosababishwa na mvua ili tutakapotoa fedha za kukarabati miradi hiyo tuwe na uhakika, hata mvua ikija miradi hiyo haitaathirika tena na mvua kuliko kukimbilia kufanya ukarabati wa muda mfupi mfupi wakati huu mvua zikiwa zinanyesha tunaweza tukakarabati, lakini hakuwezi kuwa na ubora kama ambavyo tukisubiri mvua zipungue," alisema.

Katika hatua nyingine, Chalamila alipongeza Mkuu wa Shule ya Sekondari Mvuti kwa usimamizi mzuri wa shule mpya ya sekondari inayojengwa ndani ya Kata ya Msongola kwa thamani ya Sh. 528,998,424.

"Nimekuja nikifuatilia ujenzi wa shule hii na kujionea jinsi ulivyojengwa kwa ubora wa hali ya juu kutokana na fedha zilizotolewa na serikali," alisema.

Hata hivyo, Chalamila aliagiza Zahanati ya Nzasa inayojengwa katika Kata ya Zingiziwa kwa takribani Sh. milioni 150, ifanyiwe marekebisho ikiwemo kutengeneza njia za chemchem katika eneo hilo ili ianze kutumika haraka iwezekanavyo.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, aliwataka wakandarasi na wasimamizi wengine wa miradi ya shule, kuiga mfano wa shule hiyo iliyojengwa kisasa ambayo madarasa yake yamejengwa kwa marumaru, umeme na madirisha ya alluminium na maabara za kisasa za kujifunzia.



**"Nimejionea changamoto za barabara na kwa sasa hazipitiki, hivyo basi, naelekeza ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilala, mvua zikipungua ni kuangalia mguu kwa mguu athari zilizosababishwa na mvua ili tutakapotoa fedha za kukarabati miradi hiyo tuwe na uhakika, hata mvua ikija miradi hiyo haitaathirika tena na mvua...**

# Waziri ataka Suza kuzalisha wataalamu bora

**Na Imani Mtumwa, Maelezo**

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa, amekitaka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Suza) kuendelea kutoa taaluma za fani mbalimbali ili kuhakikisha kinazalisha wataalamu bora.

Aliyasema hayo wakati akizindua Baraza la Nane la Suza juzi.

Akizindua Baraza la Nane la Suza, alisema wajumbe wote walioteuliwa ni watendaji wa serikali hivyo ni matumaini yake wajumbe hao wanaweza kufanya maamuzi mazuri ya kuendelea kufanikisha mipango na mikakati ya chuo hicho.

Alisema Zanzibar imekuwa na ufaulu mkubwa kwa wanafunzi wa sekondari, hivyo Suza inahitaji kuendelea kuwa na mipango ya kuandaa programu mbalimbali ziatakazowafanya wanafunzi hao kujifunza kupitia chuo hicho.

Pia aliwataka wajumbe hao kutumia tafiti mbalimbali juu ya miradi mikubwa ili kuleta mageuzi yanayoendana na wakati na kuisaidia serikali kukuza uchumi wa Taifa.

Waziri Lela aliwataka wajumbe hao kuhakikisha wanaendelea kutatua changamoto za kutanua miundombinu ya upatikanaji wa fani ili kuhakikisha wanafunzi kutoka sekondari kupata fursa ndani ya chuo hicho.

Aidha, aliwataka wajumbe hao kufanya kazi kwa kushirikiana na wajumbe waliopita ili kuhakikisha wanaiendeleza vyema sekta ya elimu na kuhakikisha Suza inatoa vipaumbele vya ufundi kwa upande wa Zanzibar.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Hamida Ahmad Muhammed, alimpongeza Waziri wa Elimu kwa kuharakisha kuchagua baraza jingine mara baada ya kumaliza muda kwa baraza la saba ili kuhakikisha chuo hicho kinaendelea kuzalisha wataalamu wa fani mbalimbali.

Naye Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Mohammed Makame Haji, aliwataka wajumbe wapya kutumia utaalamu katika utekelezaji wa kazi zao ili kuisadia Serikali kufikia malengo yake ya Uchumi wa Buluu.

# Kiingereza kuanza darasa la kwanza 2024

**Na Mwandishi Wetu, Chalinze**

UTEKELEZAJI wa kufundisha somo la Kiingereza kuanzia darasa la kwanza kufuatia mabadiliko ya Mtaala wa Elimu ya Msingi 2023, utaanza rasmi Januari, mwakani.

Utekelezaji huo ni hatua itakayomuandaa mwanafunzi kujiimarisha kwenye matamshi na kufanya mawasiliano vizuri kwa lugha hiyo kuanzia ngazi chini ya msingi.

Somo hilo litaanza kufundishwa darasa la kwanza badala ya darasa la tatu tofauti na ilivyokuwa katika Mtaala wa Elimu ya Msingi wa mwaka 2016.

Mwenyekiti wa Maandalizi ya mafunzo ya somo la Kiingereza kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Gastor Mapunda, aliyaeleza hayo katika mafunzo yaliyoandaliwa kwa kushirikiana kati ya Ofisi ya Rais-Tamisemi , Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania katika Programu ya Mradi wa Shule Bora ambayo inatekelezwa katika mikoa tisa ya Tanzania Bara kwa ufadhili wa Shirika la Msaada la Uingereza (UKaid) na kwa usimamizi wa Cambridge Education kwa viongozi wa elimu wa Halmashauri ya Chalinze, mkoani Pwani.

Aliwaasa walimu wa somo la Kiingereza waongeze umahiri wa kutosha ili kuleta matokeo chanya katika utekelezaji huo.

Vile vile, Profsa Mapunda aliwataka maofisa elimu wadhibiti ubora wayatambue maboresho hayo na kwenda kuyasimamia kikamilifu.

"Kwa mujibu wa mtaala, utaanza kwa wanafunzi wa elimu ya awali, darasa la kwanza na la tatu, lengo la kufanya mabadiliko hayo ni kutekeleza ahadi aliyoitoa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ya kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na Madadiliko ya Mtaala ili kuwa na sera na mitaala inayoakisi mahitaji ya sasa na baadaye.

"Katika kuzingatia maono ya Rais kwenye mabadiliko haya, tunataka kumuandaa mtoto aweze kufikia ndoto zake," alifafanua Profesa Mapunda.

Awali, Mkuza Mtaala wa somo la Kiingereza kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Neema Matingo, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwapa uelewa mpana viongozi wa elimu kuhusu mabadiliko ya mtaala huo.

"Baada ya mafunzo haya yatafuata mafunzo ya siku tano kwa ajili ya walimu mahiri wa somo la English katika Halmashauri ya Chalinze kuanzia Novemba 21 hadi 25 yanayoshirikisha wawezeshaji kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania, Chuo cha Agha Khan, Chuo cha Ualimu Vikindu na Mdhibiti Ubora wa Kanda."

Kwa upande wake, Mwalimu Hawa Waziri anayefundisha somo la Kiingereza kutoka Shule ya Msingi Magome, Kata ya Pera, Chalinze alisema mafunzo hayo yatawaweka vizuri, na kuongeza ari na ufanisi.

Alisema wanaamini baada ya mafunzo wataweza kuchambua muhtasari wa somo la Kiingereza kwa darasa la kwanza na la tatu, kuandaa na kutumia mbinu za ufundishaji wa somo hilo.

**Katika kuzingatia maono ya Rais kwenye mabadiliko haya, tunataka kumuandaa mtoto aweze kufikia ndoto zake.**

# Dondoo za wiki



Na Mwalimu Paul Masatu
Simu: +255 766 775 255

# Ondoa tabia kikwazo, jenga tabia wezeshi

LEO naomba niorodheshe baadhi ya tabia mbaya ambazo ni kikwazo kwenye mafanikio yako uwe unajua hau hujui. Yaani kama unazo tabia hizi au baadhi ya hizi, hakikisha unazishughulikia na kuziacha. Usiingie nazo mwaka mpya wa 2024.

**KUKOSA MIPANGO**

Tabia ya kutokuwa na mipango inayotekelezeka ni makosa ambayo inawezekana unayarudia kila mwaka na tabia hii inakufanya ubaki hapohapo au kukufanya hatua zako ziwe kidogo.

Mipango yako ndiyo utakayoitumia kama alama ya kwamba unachokifanya kitakufikisha kwenye malengo yako, kuna msemo unasema, usipopanga basi ujue umepanga kushindwa.

Kuishi kwa mipango kuna kutengenezea nidhamu ya matumizi sahihi ya rasilimali zako kama muda na fedha. Kuishi kwa mipango kunakufanya uweze kufanya tathmini ambayo itakusaidia kurekebisha pale ambapo umekosea.

**KUISHIA NJIANI**

Ili uweze kupata matokeo kwenye maisha, lazima kuwe na mwendelezo wa mambo (consistency). Kitendo cha kuanzisha jambo na kushindwa kulipa mwendelezo, kinafanya jambo hilo kukosa nguvu ya kuja baadaye kulikamilisha, nguvu ya kukamilisha jambo inapatikana katika mwendelezo.

**KUAHIRISHA MAMBO**

Tabia ya kughairisha au kuahirisha mambo (procrastination) ni moja ya tabia vikwazo vya mafanikio ya watu. Kughairisha ni kupanga na kila siku unasema nitatekeleza kesho.

Ukitaka mafanikio kwenye maisha, wekeza nguvu kwenye utafiti wa mambo. Na ukishaamua unatakiwa kuanza mara moja utekelezaji. Hii itakupa matokeo makubwa na kwa haraka. Kwa kifupi, kughairisha ni nguvu ya kurudisha nyuma ya mafanikio.

**KUKATA TAMAA HARAKA**

Kukata tamaa ni adui wa mafanikio. Kukata tamaa kunasababishwa na vikwazo ambavyo mtu anakutana navyo njiani.

Vikwazo vinakufumba macho ya akili yako usione mwisho wa jambo, unahitaji kuona mwisho wa jambo tangu mwanzo, ili vikwazo vinapokuja uvishinde na kusonga mbele ili kulifanikisha jambo lako.

Kimsingi,m changamoto zinapaswa kukufanya ukae chini na kuangaliua namna ya kupambana nazo au kuzigeuza fursa.

Kumbuka kisa maarufu kwamba kuna kipande cha nyama kiliziba njia ya sisimizi. Wakati kipande cha nyama kinadondoka kwenye njia yao, sisimizi wengine walikuwa upande wa pili.

Sisimizi walifikiri, wakaamua kugueza ile nyama kitoweo hata kama walikaa muda mrefu lakini walipata mlo na baada ya kulimaliza kile kipande wakaendelea na shughuli zao!

**UVIVU**

Uvivu aghalabu si kukosa nguvu ya kutekeleza jambo bali kuamua kujitenga na jambo hilo kwa kudhani ni gumu ama unataka kujipa raha.

Kwa mujibu wa Wikipedia, uvivu ni tabia ya kupenda kukaa bila kazi maalumu au kuifanya bila bidii; hali hiyo inamfanya mtu ajihisi daima na uchovu na kwamba hawezi kufanya kazi ingawa mwili wake ni mzima kabisa.

Kimsingi, uvivu ni tabia mbaya nyingine kama kughairisha mambo. Uvivu pia humkufanya mtu afanye jambo kwa ulegevu. Uvivu unakufanya ufanye jambo katika viwango vya chini (substandard), hatua ambayo haiwezi kuleta matokeo kusudiwa Kuna uhusiano mkubwa wa mafanikio ya mtu na hatua yake ya kutoendekeza uvivu.



**Kuishi kwa mipango kuna kutengenezea nidhamu ya matumizi sahihi ya rasilimali zako kama muda na fedha. Kuishi kwa mipango kunakufanya uweze kufanya tathmini ambayo itakusaidia kurekebisha pale ambapo umekosea.**

**KUTOTIMIZA AHADI**

Kukosa uwajibikaji na mwelekeo sahihi kwenye mambo uliyopanga kufanya ni tatizo lingibne kubwa. Wewe unapanga kuanza kuweka akiba, kwa mfano lakini siku zinakwenda tu hutekelezi ahadi zako mwenyewe.

Unapanga kuanza kusoma vitabu, lakini unakosa nguvu ya kutekeleza hilo. Unapanga kuanza kufanya mazoezi lakini unashindwa kutimiza hiyo ahadi yako. Tabia hii ni kikwazo kikubwa kwako.

**KUJINYIMA**

Neno 'Delay gratification' linamaanisha uwezo wa kujizuia kufanya mambo ambayo yanaonekana mazuri kwa sasa kwa ajili ya faida ya baadaye.

Yaani unajinyima starehe za muda kwa malengo ya muda mrefu, kama vile kunadhibiti hamu (appetite) yako au kiu yako kwa faida ya afya yako. Kuna watu wana kisukari, kwa mfano, na hivyo ni muhimu kwao kuacha baadhi ya vyakula kwa ajili ya afya zao. Hawa wanataka kujitenga kabisa na vyakula hivyo hata kama wanavipenda namna gani

Pia kuna wakati mtu anatakiwa kujinyima usingizi kwa saa kadhaa ili upate muda wa kusoma au kufanya kazi kama si kufanya ibada na kujinyima starehe mbalimbali kwa muda, kwa malengo makubwa ya maisha.

**KUKOSA MTIRIRIKO WA MAWAZO CHANYA**

Jiangalie kama mawazo yako yametawanyika sana. Mara unawaza hili mara lile. Unawaza bila kuwa na lengo mahsusi (You are thinking nowhere).

Kwa maendeleo yako jikite katika wazo moja, lifanyie uchunguzi, ongea na watu kuhusu wazo hilo kisha lifanyie kazi kwa bidii na maarifa kwani linaweza kukutoa hapo alipo na kukupandisha juu.

**MAWASILIANO HAFIFU**

Wakati mwingine tatizo lako ni uwezo wako mdogo katika kuwasiliana ni mdogo (poor communication). Hali hii itakufanya ushindwe kuwa na mahusiano mem ana hata kuwasilisha mapendekezo yako kwa wengine, jambo ambalo litakufanya ukose mawasialiano (connections) na wengine.

Lakini hili ni jambo la kujifunza, kuiga na kuzungumza na watu wengine.

Anza sasa kutengeneza uwezo wako wa kuwasilaiana na kujenga hoja zikaeleweka kwa watu.

**KUPENDA SANA USINGIZI**

Ni kweli kwamba kulala usingizi kwa saa zinazokubaliwa na watalaamu wa afya kwa siku, yaani kati ya saa sita hadi nane na si chini ya hapo ni jambo muhimu kwa afya yako.

Lakini ukijiona ni mtu wa kupenda sana usingizi, kwa maana ya kuuendekeza, basi ujue hilo ni tatizo. Hutotoboa na hivyo acha kuanzia sasa hiyo tabia. Usingizi usikutawale bali uutawale.

**KUTOONA MBALI**

Tabia hii inakufanya kuona vitu vinavyoonekana tu na huwezi kuona zaidi ya hapo. Yaani umejifungia ndani boksi. Lazima kila mara ufikirie mambo hata nje ya boksi. Kwamba jambo hili ninalitazama hivi, vipi nikilitazama vinginevyo! Kumsingi unakutakiwa kila mara kutafuta na kukubali kupokea mawazo mapya juu ya jambo fulani.

**KUTOKUWA NA VIPAUMBELE**

Unatakiwa kuwa na vipaumbele na kuhakikisha unavitimiza kwanza kabla ya mengine yanayoibuka. Usiishi ukiwa mtu wa kila linalokuja mbele yako wewe ndiyo hilohilo unaibuka nalo.

**MTAZAMO MBAYA/FINYU**

Usiwe mtu wa kutazama zaidi matatizo yako kuliko unavyotazama malengo yako.

Moja kati ya uwekezaji mkubwa unaotakiwa kuufanya ni kushughulika na tabia zako, hasa kuondoa tabia kikwazo na kujenga tabia wezeshi. Msingi wa mafanikio uko kwenye tabia zako zaidi.

Mwisho, endelea kukumbuka kuwa, maisha ni mchakato (process), hivyo jitihada zozote za kutafuta mafanikio kwa njia za mkato (shortcuts)haziwezi kukupa ushindi utakaodumu.

Wework Consult

Your Partner in Growth.

Jarida hili haliuzwi

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo

JARIDA

| Jumatano Novemba 22 - 28, 2023 |

# Jungu kuu






# Agizo la Waziri Mkuu wafugaji kubadilika lifanyiwe kazi sasa

UK. 12 & 13

## Elimu

# Ni aibu mtoto kupelekwa shule kwa shinikizo la polisi



**Na Reubeni Lumbagala, Kongwa**

TUPO kwenye karne ya 21, karne ya maendeleo makubwa ya sayansi ya teknolojia, karne yenye kasi ya maendeleo kwenye kila nyanja. Hata hivyo, wapo baadhi ya Watanzania wenzetu wachache, bado wanaishi maisha ya ulimwengu wa karne ya 15 kwenye karne hii ya 21.

Maisha ya karne ya 15 na pengine hadi karne ya19, hayakuweka mkazo mkubwa kwa wananchi kusaka maarifa kupitia shule kwa maana ya elimu maalumu. Elimu ya wakati huo ambayo ilimbagua sana mtoto wa kike, ilikuwa ni elimu isiyo maalumu (informal).

Ikaja ya elimu ya zama ambazo tulikuwa tupo chini ya utawala wa kikoloni iliyokuwa ya kibaguzi pia. Pamoja na ubaguzi huo, bado wazazi wengi hawakujua umuhimu wa elimu maalumu (formal education).

Hata hivyo, elimu ya darasani kwa wachache waliofanikiwa kuipata, ilisaidia sana kupata ukombozi wa kifikra hadi kufikia hatua ya kuchukua hatua kuuangusha ukoloni kwa kuanzisha harakati za kudai uhuru ili wananchi waweze kujitawala wenyewe na kufurahia maisha.

Baada ya nchi nyingi za Afrika kupata uhuru, Tanzania ikiwemo, kumekuwa na juhudi kubwa za kuinua sekta ya elimu, tena elimu isiyo ya kibaguzi, kuanzia elimu ya awali hadi elimu ya juu.

Juhudi kubwa zinazofanywa na serikali na sekta binafsi za kuinua sekta ya elimu baada ya uhuru, zinatokana na ukweli kuwa, maendeleo katika nyanja zote yanaanzia na kutegemea sana mafanikio ya sekta ya elimu. Hivyo, kabla ya kuinua sekta nyingine, ni lazima kuanza kuinua elimu, kwani elimu ndio chanzo cha mafanikio ya kila sekta ya maendeleo.

Ni kupitia elimu tunapata walimu ambao ni mama na baba wa taaluma zote, tunapata madaktari, wahandisi, maofisa ugani, makarani, madereva hadi wakulima na wafugaji wa kisasa.

Kumekuwa na ongezeko kubwa la ujenzi wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu hapa nchini ili kuongeza wigo wa udahili wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu. Lengo ni kupata wasomi wa kutosha ambao ni raslimali muhimu kwa ajili ya kuongeza kasi ya maendeleo na ukuaji wa uchumi.

Ili kuhakikisha kila mtoto anapata haki yake muhimu ya elimu, mwaka 2016 serikali ilianza kutekelezeza kwa vitendo sera ya elimu bila ada kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne.

Lakini sasa serikali imeongeza wigo hadi kidato cha sita ili watoto waweze kusoma shule bila kulipa ada ambayo ilikuwa ikiwakwaza baadhi ya wazazi na walezi wengi hasa wenye vipato vya chini katika kusomesha watoto wao.

Serikali inatoa fedha nyingi kama ruzuku ya kuendesha sera ya elimu bila ada kuanzia shule za msingi hadi kidato cha sita, hatua inayokwenda sambamba na mtazamo wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliyepata kusema kwamba "ukitaka kumsaidia mtoto wa maskini, mpe elimu."

Tukiwa tupo karne ya 21 yenye watu wenye kiu kubwa ya kusaka maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali, wapo baadhi ya Watanzania wachache ambao wanarudisha nyuma juhudi hizo kwa kuwakataza na kuwazuia watoto wao wasijiunge na elimu, hasa elimu ya sekondari baada ya kufaulu elimu ya msingi.

Baadhi ya wazazi na walezi wanafikia hatua ya kuwashauri au kuwalazimisha watoto wao wajifelishe makusudi katika mtihani wa taifa wa darasa la saba ili wasiendelee na elimu ya sekondari.

Wazazi na walezi wa aina hii ni kikwazo kikubwa dhidi ya mpango wa serikali wa kuhakikisha kila mtoto anapata haki yake ya msingi ya elimu hadi kiwango atakachoweza kufika.

Elimu imekuwa ikipewa sifa nyingi kama vile ufunguo wa maisha lakini imekuwa msaada mkubwa kwa wanufaika wengi kujitegemea baada ya kuhitimu masomo yao.

Ni jambo la kushangaza kuona licha ya utekelezaji wa sera ya elimu bila ada, bado wapo baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa hawataki au wanafanya uzembe wa kutowapeleka shule kwa wakati watoto wao.

Wapo pia wazazi wanaowashauri watoto wao waache shule ili wajishughulishe na shughuli nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji, uchimbaji madini, biashara na kazi za ndani.

Kwa kuwa serikali ina mkono mrefu na imedhamiria pasi na shaka kuhakikisha kila mtoto anapata elimu, imeamua kutumia vyombo vyake vya ulinzi na usalama kama vile askari polisi na wana mgambo kuwasaka wazazi wa watoto ambao hushindwa kuripori shule kwa wakati au kutoripoti kabisa.

Kila mwanzoni mwa mwaka shule zinapofunguliwa, viongozi wa serikali katika wilaya na mikoa hapa nchini wamekuwa wakitoa takwimu katika maeneo yao juu ya idadi ya wanafunzi ambao wameripoti na ambao hawakuripoti kwa muda unaotakiwa kisheria.

Wakati mwingine baadhi ya wanafunzi wanaoripoti kwenye shule mbalimbali, huwa ni matokeo ya matumizi ya nguvu ya ziada ya askari mgambo au polisi kuwakamata wazazi wa watoto hao.

Wakuu wa wilaya, wakurugenzi, mofisa tarafa, watendaji kata na wa vijiji kote nchini wanafanya kazi kubwa kufuatilia watoto ambao hawajaripoti shule ili waweze kuripoti shule na kuanza masomo mara moja.

Nitoe rai kwa wazazi na walezi kubadilika ili kuendana na ulimwengu tuliomo. Zama hizi ni zama za kila mtoto kupata haki yake ya elimu. Hatuwezi kuishi maisha ya mwaka 1947 katika zama hizi za sayansi na teknolojia.

Ni fedheha kubwa kwa karne ya 21 tuliyopo mtoto kusoma shule kwa msukumo wa mgambo au askari polisi na si kwa ridhaa na mapenzi ya wazazi na walezi katika kuhakikisha mtoto wao anapata haki ya elimu.

Hebu wazazi tuiunge mkono serikali yetu kwa kuwapeleka shule watoto wetu na pia kuwapatia mahitaji muhimu kama sare, viatu, madaftari na chakula ili wasome vizuri kwani kama wanavyosema wahenga, elimu ni ufunguo wa maisha.

Zoezi la uandikishaji wa wanafunzi darasa la kwanza na awali linaendelea nchi nzima sasa. Hivyo basi, wazazi na walezi wenye watoto waliokidhi sifa na vigezo vya kuandikishwa darasa la awali na la kwanza wajharakishe kwenda kuwaandikishe watoto wao kwenye shule za msingi zilizopo kwenye mitaa, vitongoji, vijiji na kata zao ili waanze masomo rasmi mwaka 2024.

Vilevile, wazazi wenye watoto waliohitimu darasa la saba wajipange kwa ajili ya kuwapeka watoto wao shule za sekondari ili waendelee na masomo yao kwa mwaka ujao wa 2024.

Mgambo na askari polisi wabaki na jukumu lao la msingi la kulinda usalama wa raia na mali zao. Hili la ufuatiliaji wa wanafunzi wanaoshindwa kuandikishwa shule na wale wanaoshindwa kuripoti shule si kazi yao na kwa kweli ni aibu. Wazazi tujiongoze wenyewe. Wazazi tubadilike.

*Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Mawasiliana yake ni: (+255) 620 800 462.*



**Kolamu**

Hamisi Kibari

## TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Haya yanachangia wanaume kuchepuka

JUMAPILI iliyopita, ilikuwa 'Siku ya Wanaume' na hivyo mijadala kadhaa kwenye makundi sogozi na vyombo vya habari, ilihusu pia masuala mbalimbali yahusuyo wanaume.

Moja ya mada iliyojadiliwa na kituo kimoja cha radio ilihusu saikolojia ya wanaume, hususani athari za masuala yanayowafanya kuvumilia maumivu kama vile kujizuia kulia kwenye misiba inayowagusa, kunyanyaswa na wake zao na mengine mfano wa hayo.

Lakini mada nyingine ambayo nimeona nitoe mchango wangu kupitia safu hii ni iliyoendeshwa na kituo kingine cha radio, iliyokuwa inajaribu kuangalia kwa nini wanaume ndio 'wachepukaji' wakubwa kwenye ndoa kulinganisha na wanawake.

Ingawa nilikuta imeshaanza, kwa kipande nilichosikiliza, wazungumzaji wengi hawakugusia yale ambayo mimi ninaamini yana mchango wake katika kuwafanya wanaume waongoze kwa kuchepuka.

Kama walivyo wengi tunaoamini katika maandiko, nianze kwa kusema kwamba kuchepuka ni kumwasi Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa sababu anayechepuka anazini.

Zinaa inakatazwa na vitabu vyote vitakatifu na dini nyingine zinakwenda mbali zaidi kwa kuliona kosa hilo ni jinai, ambalo adhabu yake kwa mtu aliyeoa, kama nchi inafuata sheria za dini hiyo, ni kifo!

Kwa hiyo ukisikia mtu anasema 'hii ni nyumba ndogo yangu', au 'yule anachepuka' basi kwa muktadha wa dini hiyo unazungumza hadharani kosa la hatari. Ni kama vile mtu aseme 'mimi ni jambazi', 'yule ni mhaini anataka kupindua nchi', 'sisi ni wauaji' na kadhalika.

Lakini, kwa faida yako msomaji nilimsikia kiongozi mmoja wa dini hiyo akisema kwamba pamoja na kuweka sheria kali kwa wazinifu, ushahidi wake ili hakimu (kadhi) apitishe hukumu ya kifo ni ngumu sana. Kwa sababu ni mpaka watu wanne wawe wameshuhudia wazinifu wawili wakiwa kwenye tendo na si, kwa mfano, kuwaona wakitoka gesti pekee!

Tuliache hilo, tuje kwenye mchango wangu, kwa nini wanaume wanaongoza kwa kuchepuka? Ninaungana na hoja nyingi zilizotolewa na wazungumzaji lakini nafasi haitoshi kuzirejea. Hata hivyo, mimi binafsi ninaamini kinachochangia uchepukaji ni watu kukimbia uhalisia wa kimaumbile!

Kwa sisi tunaoamini maandiko, mwanaume katika ndoa anahitaji vitu viwili vikubwa kutoka kwa mkewe. Cha kwanza ni heshima na cha pili ni furaha. Hivyo vikikosekana atavitafuta kwingineko. Nashangaa wanawake wengi hawafundwi hilo!

Nikianza na heshima, mwanaume kwa maumbile yake, akigundua kwamba mkewe hamheshimu, taratibu anaanza kutafuta mahala atakapoheshimiwa.

Mwenyezi Mungu aliyetuumba pia amesema kupitia maandiko matakatifu kwamba mwanaume ni kichwa cha familia kwa maana ndiye kiongozi na hayo ni maumbile aliyoumbwa nayo.

Kuhusu furaha (au niite kitulizo cha moyo), kila mwanaume mwenye ndoa, anatarajia kupata furaha kwa mkewe. Anatarajia anapotoka kwenye mahangaiko aambiwe maneno yenye furaha. Lakini anapokuwa kila mara anakumbana na malalamiko, masimango na kutoheshimiwa nyumbani, basi mwanaume huyu anatafuta atakakopata furaha.

Niliwahi kuishi Tandika Maghorofani na bwana mmoja, alikuwa Mwenyezi Mungu amemjaalia kazi nzuri na pesa haikuwa shida kwake, lakini mkewe alikuwa kero kwake kutoka na maneno. Hadi sisi majirani tukajua kwamba jamaa hana amani nyumvani kwake na kwa kweli kero za hiyo mwanamke zilikuwa zinafika hadi kwa majirani. Licha ya kuwa bosi huko kazini kwake, jamaa nyumbani hana sauti kabisa!

Anaporejea kutoka kazini, anaweza kumaliza saa mbili akiwa kwenye gari akisililiza redio au muziki 'akihofia' kwenda kukutana na kero za maneno!

Baada ya muda tukasikia huyo bwana kapata mchepuko, akakahamia huko jumla na yule mwanamke akaanza kuhaha hadi kwa waganga matapeli!

Furaha nyingine muhimu anayohitaji mwanamke ni pale anapojifungia chumbani na ubavu wake. Huko anatarajia apate mabusu na kutomaswatomaswa na mikono laini yenye bangili na hatimaye kumpumbazwa!

Nilisoma mahala wanawake wa Tanzania nao wakitamani, kama ilivyo nchi nyingine, kuwe na sheria ambayo mwanaume atakapomhitaji mkewe ambaye hajisikii kumpa unyumba, basi akitumia nguvu au kulazimisha kupata haki yake basi ashitakiwe kwa kosa la 'kumbaka mkewe'!

Kimsingi, tatizo kubwa linalosababisha michepuko mingi, liko hapa kwenye kunyimana ama kupangiana muda wa kupewa unyumba lakini ajabu katika nusu ya kipindi kile nilichosikia, hata walipokuwa wanafanya majumuisho, hili hawakuligusia.

Siku moja kiongozi mmoja wa dini alikuwa anatoa mafunzo kuhusu ndoa. Kwanza alisema mwanamke ili aende peponi, anachotakiwa ni kufanya mambo machache; ibada, kuacha maasi na kumtii mumewe.

Akasema mwanamke anapokuwa na mumewe nyumbani avae nguo za kuvutia. Akasema dini haizuii mwanamke kuvaa 'kimini' au kisuruali-soksi kinachoonesha maumbile yake lakini akasema mavazi haya yanatakiwa yavaliwe nyumbani, mbele ya mumewe na si barabarani.

**Kwa sisi tunaoamini maandiko, mwanaume katika ndoa anahitaji vitu viwili vikubwa kutoka kwa mkewe. Cha kwanza ni heshima na cha pili ni furaha. Hivyo vikikosekana atavitafuta kwingineko.**

Akasema mwanamke anayejitambua, hujipodoa, akavaa nguo za 'kutamanisha' na kutia manukato anapokuwa na mumewe ndani na huwa tayari muda wowote mumewe anapomtaka. Pigia msitari 'anapomtaka'.

Lakini ajabu, akasema wanawake wengi walio kwenye ndoa hufanya mambo kinyume. Wanapokuwa majumbani huvaa miguo ya kushindia huku wakinuka vikwapa lakini hujiremba pale wanapokwenda magengeni au kwenye vikao vya harusi!

Kiongozi huyo wa dini akasema mwanamke yeyote anayemnyima mumewe unyumba, basi ajue mumewe akilala huku amekasirika basi malaika humlaani mwanamke huyo usiku mzima hadi asubuhi.

Alipoulizwa kuhusu wanaume wasiowapa unyumba wake zao, akasema ingawa wapo lakini ni wachache kulinganisha na wanawake na ndio maana maandiko hayajamzungumzia mwanaume katika hilo.

Akasema kesi nyingi za migogoro ya ndoa ambazo zimefika kwake, asilimia 90 ni za wanawake kuwanyima au kuwapa unyumba kwa nadra waume zao kwa visingizio vya 'sijisikii', 'nimechoka' na sababu nyingine zisizo za kisheria kama kuwa katika hedhi au ugonjwa.

Kisha akasema kwamba kimsingi, kunapofanyika tendo la ndoa, mwanamke akifika kileleni, ladha anayopata ni zaidi ya asilimia 90 ya anayopata mwanaume.

Kisha akafafanua:

"Mwanamke akishapata hizo asilimia 90 za 'raha' anaweza akakaa hata mwezi bila kuhitaji tena.

Lakini mwanaume mwenye viasilimia vyake 10 au chini ya hapo, huhitaji unyumba mara kwa mara.

Akasema bahati nzuri, maumbile ya mwanamke yanamruhusu kumpa unyumba mumewe hata kama hajisikii kabisa lakini si kinyume chake."

Ukweli mwingine tunaojifanya kuukimbia ni kwamba mwanaume kwa asili haridhiki na mke mmoja (polygamous by nature) na ndio maana mila za mababu na baadhi ya dini zinaruhusu mwanaume kuoa zaidi ya mke mmoja kama atawamudu kwa hali na mali na kufanya uadilifu.

Kutokana na asili hiyo, wanaume, ingawa si wote, ndio maana wanaweza kuchepuka lakini bado wakatimiza haja zote na upendo kwa wake zao wa ndoa.

Katika kesi moja ya ndoa niliyowahi kushiriki, mke alilalamika baada ya kugundua kwamba mumewe anachepuka, tena si mchepuko mmoja bali zaidi. Kikao kilipomhoji mlalamikaji, alikiri kwamba tatizo ni mumewe kuwa na michepuko tu lakini hakuna kilichopungua.

Kwamba unyumba anapata kama kawaida, mahitaji ya nyumbani na watoto zikiwemo ada ni kama kawaida.

Hali ya wanaume kutoridhika na mke mmoja si kwa wanadamu pekee bali hata wanyama. Majuzi niliponunua mashine ya kutotolesha vifaranga, mtaalamu aliniambia kwamba nikienda kununua mayai kwa mfugaji, nihakikishe wastani uwe si chini ya jogoo moja kwa kuku majike sita ili kupata matokeo mazuri.

Vilevile katika jamii nyingi, ikiwemo Tanzania, wanaume ni wengi kuliko wanawake na hawa wote wanahitaji huduma za wanaume.

Mhubiri mmoja wa dini ya Kiislamu, Dk. Zakir Naik, alipotembelea Marekani aliulizwa kwa nini Uislamu unaruhusu ndoa za mitara. Muulizaji akasema ndoa hizo ni kumdhalilisha mwanamke.

Dk. Naik akajibu kwamba ndoa za mitara ndizo zingejibu tatizo la Marekani la kuwa na wanawake wengi waliokosa waume badala ya kupigia debe ushoga.

Akasema licha ya sensa kuonesha kwamba Marekani ina wanawake wengi kuliko wanaume, baadhi ya wanaume hao wachache miongoni mwao ni mashoga, wengine ni mapadri wa madhehebu ambayo haruhusu kuoa na wengine ni wafungwa.

Akasema kutokana na hali hiyo, ndoa za mitara zinapopigwa vita na kuonekana ni unyanyasaji (au huku kwetu kuonekana ushamba au kitu kilichopitwa na wakati), basi idadi kubwa ya wanawake kutokana na wingi wao watabaki kuwa public property (mali ya Umma).

Dk. Naik naye akahoji" "Sasa ni lipi jema, kupoteza kidogo kummiliki mwanaume peke yako au kuwa mali ya umma?"

Ninachosisitiza hapa ni wanawake kuhakikisha wanawapa heshima na furaha wanaume zao na kwa kufanya hivyo michepuka itapungua sana.

Pia kwa wanaume ambao dini au mila zinawaruhusu kuoa wake zaidi ya mmoja, wasione kama ni ushamba, wawanusuru wanawake walipokosa ndoa mitaani kwa kuwaoa. Kama wanaweza kuwahudumia kama nyumba ndogo zao, hakuna sababu ya kuzini wakati wanaweza kuhalalisha.

## Siasa



# Agizo la Waziri Mkuu wafugaji kubadilika lifanyiwe kazi sasa

## ■ Waache kuchunga, wafuge

**Na Hamisi Kibari**

MOJA ya jambo jema lakini linalogeuka kuwa kero na tatizo kubwa nchini ni namna ya kudhibiti ongezeko la makundi ya mifugo.

Nchi yetu inatajwa kuwa nchi ya pili Afrika kwa wingi wa mifugo baada ya Ethiopia. Takwimu zilizowahi kutolewa takribani miaka miwili iliyopita zilionesha kwamba Tanzania inakadiriwa kuwa na ng'ombe milioni 33.9 ikiifuata Ethiopia yenye ng'ombe milioni 60.39.

Takwimu hizo pia zilionesha kuwa wakulima wadogo wadogo wana mbuzi milioni 24.5, kondoo milioni 8.5 na kuku milioni 75.1 huku wakulima wakubwa wakiwa na mbuzi milioni 33.347, kondoo milioni 24.236 na kuku milioni 12.6.

### TUNAHITAJI MIFUGO

Kimsingi, tunahitaji mifugo kwa sababu ya faida zake kwetu ambazo ni kutupa mbolea, nyama, maziwa, siagi na jibini. Lakini pia tunapata mazao mengine kama ngozi, kwato na mifupa kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kama viatu, mikoba, vishikizo na sahani zinazotokana na mifupa.

Lakini kikubwa, ufugaji ni shughuli ya kiuchumi inayoajiri Watanzania wengi kuanzia wafugaji wenyewe hadi watu wanaojishughulisha na mazao yatokanayo na mifugo.

### UFUGAJI WA KIZAMANI

Lakini kutokana na ufugaji wa kizamani au wa mazoea, idadi ya watu imekuwa ikiongezeka na idadi ya mifugo imekuwa ikiongezeka pia.

Kutokana na kuongezeka kwa makundi ya mifugo, maeneo ya asili ya wafugaji kama vile Usukumani na Umasaini, yamekuwa hayawezi tena kuhimili idadi kubwa ya mifugo na hivyo wafugaji wamelazimika kuhamia maeneo mengine ambayo awali yalikuwa hayana kabisa au yakiwa na wafugaji wachache.

Baadhi ya mikoa ambayo kwa sasa ina makundi makubwa ya wafugaji waliohamia kwenye maeno hayo katika miaka ya karibuni ni Morogoro, Pwani na Lindi.

Wingi wa mifugo umekuwa ukileta athari katika uharibifu wa misitu lakini pia kusababisha migogoro isiyokwisha baina ya wafugaji ambao wengi ni wahamiaji na wakulima ambao ni wenyeji.

Kumbukumbu zinaonesha kwamba Mkoa wa Morogoro ni moja ya mikoa ambayo kwa muda mrefu umekuwa ukigubikwa na migogoro baina ya wafugaji na wakulima na wakati mwingine kushasababisha maafa kwa maana ya vifo vya watu.

Hata hivyo, tatizo la migogoro inayopindukia kwenye machafuko inazidi kusambaa katika mikoa mingine. Mwezi Septemba mwaka huu kulikuwa na habari zinazoonesha kwamba vurugu baina ya wafugaji na wakulima katika Kijiji Matekwe Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi na Kijiji cha Tinganya wilayani Tunduru mkoani Ruvuma zilisababisha mauaji ya watu watatu.

Ni kutokana na hali hiyo, hivi karibuni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema kitendo cha wafugaji kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima ni uvunjaji wa sheria. Akasisitiza kwamba serikali haitavumilia vitendo hivyo.

### HATUA ZICHUKULIWE

Ni kutokana na hilo, Waziri Mkuu anawataka viongozi wa kiserikali kuanzia watendaji wa kata hadi wakuu wa mikoa likiwemo jeshi la polisi kuchukua hatua za kisheria pale wafugaji wanapoingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima.

Waziri Mkuu ametoa agizo hilo wakati akizungumza na wananchi kwenye vijiji vya Nanjaru na Mkaranga vya Kata ya Nambilanje na Kijiji cha Nankonjera kilichopo Kata ya Namichiga akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa wilayani Ruangwa, mkoani Lindi.

Waziri Mkuu anasema migogoro baina ya wakulima na wafugaji haina tija na serikali haitaki kuiona ikiendelea. Anasema kati yao hakuna mwenye haki zaidi ya mwingine, hivyo, kila mmoja aweke mpango kazi ambao hautaathiri upande wowote.

### WAFUGAJI WABADILIKE

Waziri Mkuu ameagiza na wadau wakiwemo maofisa kutoka wizara husika wanapaswa

Siasa



kufanyia kazi mara moja ni kuwataka wafugaji wafuge mifugo yao kulingana na ukubwa wa maeneo yao ya malisho.

"Kilimo ni maisha, kilimo ni biashara, kilimo ni fedha na vivyo hivyo ufugaji ni maisha, ufugaji ni biashara na ufugaji ni fedha, hivyo kila mkulima alime kulingana na ukubwa wa eneo lake na mfugaji afuge mifugo kilingana na ukubwa wa eneo lake na malisho. Sisi sote ni Watanzania na tunataka utajiri. Wakulima na wafugaji waheshimiane kwani wote ni Watanzania," anasema Waziri Mkuu.

Anachosema hapa Waziri Mkuu ni wafugaji kusaidiwa, kuhamasishwa na ikibidi kulazimishwa kufuga kisasa kwa maana ya kupunguza mifugo na kufuga kisasa, hatua inayohusisha kulima malisho kwa ajili ya mifugo yao.

"Wafugaji badilikeni fugeni kisasa, msione fahari kuwa na idadi kubwa ya mifugo ambayo mnashindwa kuihudumia. Fugeni mifugo michache ambayo mtaihudumia vizuri na kuiuza kwa gharama kubwa."

Kadhalika Waziri Mkuu anawataka watendaji wa vijiji kabla hawajagawa maeneo kwa wafugaji wahakikishe idadi ya mifugo waliyonayo na washirikishe serikali ya kijiji na wananchi.

### KIBURI CHA WAFUGAJI

Tatizo ambalo limekuwa likisemwa kwamba linawapa kiburi wafugaji na hata Waziri Mkuu aliligusia ingawa si kwa uwazi mkubwa ni kwamba wamekuwa wakitumia pesa kufanya lolote ikiwemo kuingiza mazao yao kwenye mashamba ya wakulima!

Imekuwa ikidaiwa kwamba kutokana na uwezo wa kifedha ambapo mfugaji wanaweza kuuza mifugo muda wowote bila kusubiri msimu kama ilivyo kwa wakulima, wafugaji wamekuwa wakifanya makosa na hatua zisichukuliwe dhidi yao kutokana na 'kutembeza' fedha.

### KUMALIZA MISITU

Ingawa Waziri Mkuu anazungumzia zaidi wafugaji kusababisha migogoro baina yao na wakulima, lakini wingi wa mifugo unasababisha pia uharibifu katika misitu.

Mwaka 2022, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack aliwaambia waandishi wa habari na mashirika yanayohifadhi misitu waliomtembelea ofisini kwake akiwemo mwandishi wa makala haya kwamba wafugaji ni tatizo.

Alisema alishangaa kuona wafugaji wa jamii ya Wasukuma wanaotuhumiwa kumaliza misitu Shiyanga wakiwa Lindi. Kabla ya kuhamiishiwa Lindi, Telack alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga.

Akizungumzia umuhimu wa misitu, Telack anasema kilimo tunachosema ni uti wa mgongo kitashindikana kama hatutakuwa na misitu kwa kuwa kilimo chetu bado kwa sehemu kubwa kinategemea mvua na kwamba misitu ina nafasi kubwa ya kuvuta mvua na kulinda vyanzo vya maji.

"Sasa hivi tunasema Lindi ina misitu mingi. Ni kweli, lakini kama isipotunzwa, misitu tunayoizungumzia leo haitakuwepo (kesho)," anasema.

Faida nyingine ya misitu kwa mwanadamu na viumbe hai wengine ni kunyonya hewa ukaa na kutoa hewa safi, kuwa makazi ya viumbe mbalimbali na ndani ya misitu hupatikana miti-dawa, miti ya mbao na miti kwa ajili ya nishati ya kupikia (mkaa na kuni).

Kiuchumi, misitu huwezesha ufugaji wa nyuki lakini pia misitu, kama ilivyotajwa hapo juu hutoa mbao za aina mbalimbali na nishati za mkaa na kuni.

Inaelezwa kwamba asilimia takribani 45 ya misitu ya Tanzania iko katika ardhi za vijiji na hii ndio inayoharibiwa zaidi kwa kukatwa kwa njia isiyo endelevu sambamba na kuvamiwa na makundi ya mifugo kwa ajili ya malisho.

### NG'OMBE MILIONI 10 WALIOBORESHWA

Mwaka jana, wakati wa maonesho ya Nanenane kitaifa mkoani Mbeya, Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango aliambiwa kwamba endapo wafugaji nchi nzima watatumia ng'ombe walioboreshwa, Tanzania itahitaji kuwa na ng'ombe milioni 10 pekee wenye kilo za nyama na kutoa maziwa kama yanayozalishwa na ng'ombe wanaokadiriwa kuwa milioni 33 na ushei nchini.

Huo ulikuwa ni mtazamo wa Mohamed Mbogo, Mkurugenzi wa mashamba ya ng'ombe ya Mbogo Ranches yaliyoko Mbarali mkoani Mbeya na Ubena Zomozi, Chalinze.

Mbogo alitoa maelezo hayo kwa Makamu wa Rais, alipotembelea banda lao. Katika maonesho hayo, shamba la Mbogo lilionesha namna ng'ombe wa asili wanavyokuwa na uzito mdogo kulinganisha na walioboreshwa.

Alionesha ng'ombe wa asili wa miaka miwili akiwa na uzito kilo 196, lakini aliyeboreshwa wa umri huo huo kwa dume la boran akiwa na uzito wa kilo 347.

Alionesha pia ng'ombe aina ya boran aliyeboreshwa kwa kutumia mbegu ya Sussex mwenye umri wa mika miwili lakini akiwa na kilo 451.

Shamba hilo pia lilileta ng'ombe wa mbegu wa boran wa miaka mitatu mwenye na uzito wa kilo 625.

Alishauri Watanzania kuchangamkia kufuga ng'ombe aina ya boran kwa sababu kimsingi ni ng'ombe wa asili aliyeboreshwa.

"Huyu ng'ombe ametokana na ng'ombe wa asili, anavumilia magonjwa na kuchunga malisho yoyote kama ng'ombe wa asili," alisema.

Alisema wenzetu katika nchi jirani ya Kenya ambako ndiko walichukua mbegu hiyo wamenufaika sana na aina hiyo ya ng'ombe.

Mbogo alionesha pia aina takribani nne za mbuzi, kuanzia wa asili na walioboreswa huku hata kwa kuangalia kwa macho wale wa asili wakionekana wadogo kulinganisha na walioboreshwa ingawa wote wana umri mmoja.

Mbuzi walioboreshwa alisema wanatokana na mbegu ya Galla-goat ambayo asili yao ni Somalia.

"Kwa hiyo hata mbuzi wetu tunaweza kuwaboresha kwa kuchanganya mbegu na kufanya ufugaji wenye tija," alisema Mbogo.

Mfugaji huyo alimshukuru Rais Samia kwa hatua ya kulitaka Shirika la Ranchi za Taifa (Narco) kuona namna nzuri ya kutumia mashamba yake 14 yenye ukubwa wa zaidi ya hekta 600,000 kwa tija kuliko ilivyo sasa.

Wakati Makamu wa Rais alipopita kwenye banda lake, Mbogo alimwomba ikiwezekana wafugaji binafsi kama yeye wagawiwe mashamba hayo. Alipozungumza na mwandishi wa makala haya, Mbogo alisema wafugaji wengi wa Tanzania wanachunga ng'ombe badala ya kufuga na kwamba umefika wakati wabadilike.

Ni vyema wadau na wizara husika kuhamaisha maarifa kama ya akina Mbogo kwa wafugaji wetu, wakianza na wale wakubwa.

### MATUMIZI BORA YA ARDHI

Ni bora pia vijiji visaidiwe na serikali kuhakikisha kila kimoja kinapimwa na hatimaye kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Kijiji kinapokuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi maana yake ni kwamba kunakuwa na eneo linalotengwa kwa ajili ya makazi, eneo kwa ajili ya shughuli za michezo, eneo la ofisi na huduma za kijamii ikiwemo shule na vyuo, eneo la mashamba, eneo la msitu wa kijiji na neo la malisho.

Maeneo haya yanatakiwa kutunzwa na kufanya shughuli iliyokusudiwa.

Isiwe pia kama Halmashauri ya Bagamayo ambayo miezi michache iliyopita wafugaji waliwalalamikia baadhi ya viongozi wa vijiji kuwa sehemu ya migogoro kati yao na wakulima inatokana na kuhodhi na kuuza maeneo yaliotegwa kwa ajili ya malisho ya mifugo kwa wawekezaji.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa mkutano na Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash, aliyeamua kusikiliza kero za wafugaji hao, walisema mapigano kati yao na wakulima yamekuwa yakichochewa na viongozi wa vijiji kutokana na kuuza maeneo ya malisho kwa wawekezaji kinyume cha taratibu.

Jamii



# Umasikini na maendeleo ya Tanzania - 2

**Na Dk. Felician Kilahama**

NAMSHUKURU Mungu kwa namna anavyotujaalia amani pamoja na zawadi ya uhai na afya njema Watanzania wote.

Huu ni mwendelezo wa makala inayofafanua kuhusu kupima maendeleo/mafanikio ya Tanzania kwenye mizania moja na mataifa tajiri au yaliyoendelea kuwa pengine si jambo sahihi.

Sehemu ya kwanza ilimalizika kwa kuonesha kuwa wale wageni kutoka Ulaya waliokuja huku kwetu wakijulikana ni 'wavumbuzi' au 'wamisionari' walikuja Afrika kati ya Karne ya 14 na 18 wakitanguliwa na Waarabu kutoka Mashariki ya Kati waliofika Afrika tangu karne ya saba.

Pamoja na mambo mengine, wazungu kutoka Ulaya waligundua kuwa Afrika halikuwa bara lililo gizani bali limesheheni rasilimali, watu wenye nguvu na uwezo wa kufanya kazi pamoja na maliasili za kutosha.

Mataifa ya Ulaya yaliyokuja Afrika ni pamoja na Ujerumani, Ureno, Uingereza, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Hispania, na mengineyo. Kitu cha kwanza walichokifanya ni kugawana maeneo ya kutawala ili waweze kunufaika zaidi na raslimali zetu na wasigombane wao kwa wao.

Baada ya kugawana maeneo ya bara letu kati yao; mipaka ikawekwa na mataifa ya Afrika yakawa kwenye ramani kama walivyokubaliana hao wageni. Mipaka hii kwa sehemu kubwa ndio inayotumika hadi leo.

Wakoloni hao walifanikiwa kwa sababu walikuwa na nguvu za kivita, kimaarifa na kimiuondombinu kuwazidi mababu zetu hivyo, wakaweza kutekeleza azma yao barani Afrika kiulaini!

Hata hivyo, halikuwa jambo rahisi maana wakoloni walikumbana na upinzani mkali katika maeneo mbalimbali ikiwemo Tanzania kama vita vya Majimaji Songea, Mkoani Ruvuma na kule Kenya wakakumbana na vita vya Maumau.

Kwa hapa Tanzania, mbali na Majimaji, kulikuwepo mapambano sehemu nyingine nchini mathalani, kwa Chifu Mkwawa, Iringa kwa Chifu Milambo kule Tabora na sehemu nyinginezo.

Kama ilivyokwisha dokezwa, wakoloni walikuwa na nguvu kwa sababu mataifa ya Ulaya na Amerika wakati huo (karne ya 18), walishajijengea uwezo wa kutosha, kitaaluma na miundombinu ya usafiri na usafirishaji kama vile 'merikebu'. Isitoshe walikuwa na silaha za moto kama bunduki na risasi za kutosha.

Kwa upande mwingine, inafahamika kwamba Waarabu walianza kufanya biashara ya watumwa tangu karne ya saba na biashara hiyo iliendelea hadi miaka ya 1960 wakati baadhi ya nchi za kiafrika zilipoanza kupata uhuru.

Njia kuu mbili zilitumika katika biashara hiyo ya utumwa; kutoka Pwani ya Afrika hadi Mashariki ya Kati (Middle East). Pili, ni ile ya "trans-Saharan Caravan Traffic" ikiungana na biashara ya watumwa iliyoanzia Afrika Magaharibi kwenda Amerika Kaskazini na Kati (nchi za Caribbean) hadi Brazil (Amerika ya Kusini).

Vilevile, kupitia Pwani ya mashariki mwa Afrika, watumwa walipelekwa Uarabuni.

Kwa upande wa Afrika Mashariki, biashara ya watumwa ilianzia Kaskazini hadi kusini mwa Afrika kwa kuunganisha maeneo ya Ethiopia na Eritrea pamoja na Somalia na kuteremkia Afrika Mashariki hadi eneo la 'Maziwa Makuu' mpaka Msumbiji.

Historia inaonyesha kuwa kutoka Afrika watu kati ya milioni 12 hadi 15 walipelekwa sehemu mbalimbali duniani.

Pamoja na hayo yote kufanyika Afrika, bado mataifa ya Ulaya yaliyotawala nchi mbalimbali; harakati hizo zilikuwa ni sehemu ya mikakati yao hasa ya kujiletea maendeleo yaliyochochewa na kukua kwa viwanda/uchumi takribani zaidi ya miaka 300 iliyopita.

Hali hiyo ilichangia sana kuwafanya waje Afrika baada ya kugundua kuwa zilikuwepo fursa za kutosha. Hivyo, Wakoloni walichukua rasilimali nyingi katika maeneo mbalimbali ya Afrika.

Pamoja na nguvukazi kubwa kuchukuliwa kama watumwa, pia walichukua madini mbalimbali pamoja na rasilimali nyingi kama madini, vito vya thamani, mbao, magogo na nguzo kutoka kwenye misitu ya asili.

Vilevile walipora mazao na malighafi za viwanda mathalani, pamba, kahawa, ngozi za wanyama kama chui, simba, mamba na kadhalika; meno ya tembo na faru pamoja na rasilimali nyinginezo walizoziona kuwa zina thamani kiuchumi na kijamii.

Kimsingi, wakoloni waliweza kuyafanya hayo kutokana na uwezo wa kimaendeleo na kiuchumi waliokuwa wameufikia. Wakati huo Afrika ilikuwa kwenye hali isiyoeleweka kielimu na kimaendeleo.

Maendeleo yaliyofanyika kwenye 'makoloni' husika, yalilenga kuwawezesha wakoloni kusafirisha malighafi, madini na bidhaa nyinginezo kutoka Afrika. Mathalani, hapa kwetu, Wajerumani na Waingereza walijenga reli ya kati hadi Mwanza na Kigoma; pia mpaka Arusha na Tanga na baadaye Kaliua mpaka Mpanda. Vilevile, ilikuwepo reli kutoka Tanga hadi eneo la 'Zigi' kwenye Msitu Asilia wa Amani Wilayani Muheza.

Kadhalika, zilijengwa bandari kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi na katika Maziwa Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa) kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa bidhaa/malighafi na watumwa kwenda maeneo kusudiwa nje ya Afrika.

Je, hali kama hiyo iliashiria nini kwa mustakabali mzima kwa Afrika? Jitihada za mataifa ya Ulaya kuwa na makoloni katika Afriaka zilipelekea Bara letu kudhoofika kijamii, kiutamaduni na kimaendeleo.

Kupitia Kitabu kilichoandikwa na 'Walter Rodney (1972); mwandishi alieleza kinaganaga jinsi Afrika ilivyonyonywa kimakusudi na kutoendelezwa na wakoloni. Moja ya hoja zake kuu katika kitabu hicho, inasisitiza kuwa "Afrika iliendeleza mataifa ya Ulaya kwa kasi kubwa na wakati huohuo, mataifa ya Ulaya yaliifanya Afrika kuwa duni kwa takribani kasi hiyohiyo."

Tuseme nini juu ya hali hiyo? Ni hali ambayo haikutarajiwa maana kwa miaka mingi, Afrika ilidumaa kwa kupungukiwa nguvukazi yake muhimu pamoja na kuporwa kwa rasilimali zake muhimu hususani maliasili kama misitu, madini, wanyamapori na nyinginezo kutokana na dhamira ya wakoloni kuendeleza mataifa yao.

Tulipopata uhuru Desemba 9, 1961, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa kwanza wa nchi yetu, alitangaza mapambano ya kitaifa dhidi ya maadui watatu; maradhi, ujinga na imaskini.

Hivyo, ikawa ndiyo mwanzo wa juhudi za kujiletea maendeleo baada ya kutawaliwa/kudhoofishwa na wakoloni kwa miaka mingi. Vilevile, akatahadharisha kuwa Ulaya wameendelea sana wakati sisi tupo nyuma. Hivyo akasema tufanye kazi kwa bidii na maarifa kiasi kwamba Ulaya na Amerika wakiwa wanatembea sisi tukimbie tena bila kuchoka.

Taifa linatimiza miaka 62 tangu tujitawale na wakati huohuo bado tunapambana na maadui walewale kwa kiasi kikubwa.

Ndiyo, tumepiga hatua kiasi katika utoaji wa huduma za jamii na miundombinu katika sekta za afya (maradhi), elimu (ujinga) na uchumi (umaskini) lakini bado hatujfikia viwango takiwa ili kukidhi mahitaji kwa watanzania wote.

Bado mengi yanatakiwa kufanywa na kuendelezwa katika kukuza uchumi wa mtu mmojammoja, jamii na taifa zima kwa ujumla.

Kama taifa ni muhimu tuzidi kuiunga mkono serikali inavyopambana katika kuhakikisha kila mmoja wetu anapata riziki yake kila siku, iwe ni wakulima, wafugaji, wafanyakazi wa umma na sekta binafsi; wafanyabiashara na wajasiliamali.

Kwa kuwa viongozi wana mchango mkubwa katika kuharakisha au kurudisha nyuma maendeleo yetu, tunapoelekea kwenye chaguzi zijazo tuwe makini pia katika kuhakikisha tunapata viongozi watakaotanguliza maslahi ya nchi yetu mbele na si matumbo, uchoyo na ubinafsi wao.

Kwa maneno mengine, kila mmoja apambane ili kujitoa katika usemi wa "mradi mkono uende kinywani"; ukimaanisha kwamba mtu apate chakula mengineyo yatafuata. Nchi yetu bado ina raslimali nyingi zinazoweza kuharakisha maendeleo yetu ya kiuchumi.

Kwa hiyo ukiangalia, bado matatizo yetu ya leo yana kiini chake kwenye minyororo ya kikoloni kwani licha ya kutupatia uhuru wa bendera, wameendelea kutubana kwenye eneo la uhuru wa kiuchumi.

Hivyo, taifa linajikuta katika hali yenye changamoto kadhaa za kiuchumi, kitamaduni, kimaadili na kimaendeleo kwani mataifa yaliyoitawala Afrika, kama ilivyokwishakuelezwa, hawakuja kwa mtazamo wa kuendeleza Afrika; bali kujikwamua kiuchumi na kuendeleza mataifa yao.

Na kwa kuwa wakoloni Hawa walishaonja na kufahamu maendeleo maana yake nini; hawakuwa na ajizi isipokuwa kufanya kweli ili wajiendeleze zaidi kupitia nguvukazi kutoka Afrika pamoja na rasilimali nyinginezo nyingi kulingana na uwezo waliokuwa nao wa kuzichukua maana hapakuwepo na kizuizi cha maana.

Hata hivyo, maandiko matakatifu yanatutahadharisha kuwa "iwapo misingi ikiharibika, mwenyehaki atafanya nini?" Kabla ya wakoloni kuja Afrika, kulikuwepo misingi iliyowezesha wakazi wake kuyamudu maisha yao.

Kitendo cha kutawaliwa ikawa ndiyo chimbuko la kuharibika kwa misingi husika: kwa hali hiyo mwenye haki (mwananchi) atafanya nini? Ndiyo maana mwandishi wa kitabu cha 'How Europe Underdeveloped Africa' Walter Rodney (1972), akafafanua mambo yalivyokuwa yakuisababishia Afrika kuzorota kiuchumi na kimaendeleo; kwa spidi ileile ya kuondoka kwa rasilimali Afrika na kuzipeleka Ulaya na kwingineko duniani.

*Itaendelea*



# Dalili 10 za saratani zisizotambulika kirahisi

WATU wengi wanaposikia neno saratani, huhusisha na ugonjwa hatari na matokeo mabaya.

Lakini tangu miaka ya 1970, kiwango cha kuishi kimeongezeka kwa sababu tatu hasa kwa utambuzi wa mapema.

Na hakika, saratani nyingi zinaweza kutibiwa na matokeo mazuri kwa mgonjwa zinapogunduliwa kabla hazijakua sana.

Tatizo ni kwamba mara nyingi watu wengine hupuuza baadhi ya dalili ambazo zinaweza kuwa muhimu kwa uchunguzi wa mapema.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Shirika la Cancer Research UK, zaidi ya nusu ya Waingereza kwa wakati fulani, wamekumbwa na moja ya dalili zinazoweza kuashiria uwepo wa saratani, lakini ni asilimia mbili tu walidhani wanaweza kuugua ugonjwa huo na zaidi ya theluthi moja, walipuuza kabisa na hawakwenda kumuona daktari.

Katriina Whitaker, Mtafiti katika Chuo Kikuu cha London na Mwandishi Mkuu wa utafiti huo, anasema: "Baadhi wanadhani hatupaswi kuwahimiza watu kuwa na shauku kujua hali za afya zao, lakini tuna shida na watu ambao wanaona aibu kwenda kwa daktari kwa sababu wanaamini kwamba watapoteza muda na kupoteza rasilimali za mfumo wa afya bila manufaa.

Anaongeza: "Tunatakiwa kutuma ujumbe kwamba ukiwa na dalili ambazo haziondoki, hasa zile zinazoonekana kuwa ni dalili za tahadhari, usipuuze, nenda kwa daktari kutafuta msaada,"

Dalili 10 za jumla za saratani ambazo kulingana na Jumuiya ya Saratani ya Amerika, mtu hapaswi kuzipuuza.

**1. KUPUNGUA UZITO BILA SABABU**

Watu wengi walio na Saratani, hupoteza uzito wakati fulani.

Unapopoteza uzito bila sababu yoyote, inaitwa kupoteza uzito usiojulikana.

Kupungua kwa uzito usioelezewa kwa kilo 5 au zaidi inaweza kuwa ishara ya kwanza ya saratani.

Hii hutokea mara nyingi zaidi katika saratani ya kongosho, tumbo, umio, au mapafu.

**2. HOMA**

Homa ni ya kawaida sana kwa wagonjwa walio na saratani, ingawa hutokea mara nyingi zaidi baada ya saratani kuenea kutoka pale ilipoanzia.

Karibu kila mtu aliye na Saratani, atapata homa wakati fulani, haswa ikiwa saratani au matibabu yake yataathiri mfumo wa kinga. Homa inaweza kuwa ishara ya mapema ya saratani, kama vile leukemia au lymphoma.

**3. UCHOVU**

Uchovu ni mwingi ambao hauishi wakati wa kupumzika. Inaweza kuwa dalili ya saratani inavyoendelea.

Hata hivyo, katika saratani nyingine, kama vile ya damu, uchovu unaweza kutokea mwanzoni.

Baadhi ya saratani za koloni au tumbo zinaweza kusababisha upotezaji wa damu ambao hauonekani wazi.

Hii ni njia nyingine ambayo saratani inaweza kusababisha uchovu.

**4. MABADILIKO YA NGOZI-**

Pamoja na saratani ya ngozi, saratani nyingine zinaweza kusababisha mabadiliko ya ngozi ambayo yanaweza kuonekana. Ishara na dalili hizi ni pamoja na:

- Kuweka weusi kwenye ngozi (hyperpigmentation)
- Ngozi na macho kuwa na manjano (jaundice)
- Uwekundu wa ngozi (erythema). Kuwasha
- Ukuaji wa nywele kupita kiasi

**5. MABADILIKO YA TABIA YA TUMBO AU KUFANYA KAZI KWA KIBOFU**

Kufunga choo, kuhara au mabadiliko katika umbo la kinyesi kwa muda mrefu inaweza kuwa ishara ya saratani ya koloni.

Kwa upande mwingine, maumivu wakati wa kujisaidia haja ndogo, damu kwenye mkojo au mabadiliko katika utendaji wa kibofu cha mkojo (kama vile kujisaidia zaidi au chini ya mara kwa mara) yanaweza kuhusishwa na saratani ya kibofu cha mkojo au kibofu.

**6. VIDONDA VISIVYOPONA**

Watu wengi wanajua kwamba fuko ambazo hukua, kuumiza au kuvuja damu, zinaweza kuwa dalili za saratani ya ngozi, lakini pia tunapaswa kuwa waangalifu kwa majeraha madogo ambayo hayaponi kwa zaidi ya wiki nne.

Kidonda cha mdomo ambacho hakiponi, kinaweza kuwa kwa sababu ya saratani ya mdomo.

Mabadiliko yoyote katika kinywa chako ambayo hudumu kwa muda mrefu yanapaswa kuchunguzwa mara moja na daktari au daktari wa meno.

Vidonda kwenye uume au uke vinaweza kuwa dalili za maambukizi au saratani ya hatua ya awali, na vinapaswa kuchunguzwa na mtaalamu wa afya.

**7.KUTOKA DAMU**

Kwa upande mwingine, ikiwa damu inaonekana kwenye kinyesi (ambayo inaweza kuwa na rangi nyeusi sana), inaweza kuwa ishara ya saratani ya koloni au saratani ya puru.

Saratani ya shingo ya kizazi ya endometriamu (kitambaa cha uterasi), inaweza kusababisha kutokwa na damu kusiko kwa kawaida katika uke.

Pia, damu katika mkojo, inaweza kuwa ishara ya saratani ya kibofu au figo.

Kutokwa na damu kutoka kwa chuchu, kunaweza kuwa ishara ya saratani ya matiti.

**8. UGUMU AU UZITO MAHALI POPOTE KWENYE MWILI**

Saratani nyingi zinaweza kuhisiwa kupitia ngozi.

Saratani hizi hutokea hasa kwenye matiti, tezi dume, tezi (lymph nodes) na tishu laini za mwili. Uzito au ugumu unaweza kuwa ishara ya mapema ya saratani.

**9. UGUMU WA KUMEZA**

Ukosefu wa chakula unaoendelea au ugumu wa kumeza, inaweza kuwa dalili za saratani ya umio (mrija unaoelekea kwenye tumbo), tumbo au koromeo (koo).

Hata hivyo, kama dalili nyingi kwenye orodha hii, mara nyingi husababishwa na sababu nyingine isipokuwa saratani.

**10. KIKOHOZI CHA KUDUMU AU SAUTI YA KUKWARUZA**

Kikohozi cha kudumu kinaweza kuwa ishara ya saratani ya mapafu.

Inashauriwa kumtembelea daktari ikiwa umekuwa ukiugua kwa zaidi ya wiki tatu.

Wakati huo huo, sauti ya kukwaruza inaweza kuwa ishara ya saratani ya zoloto (sehemu ya mwanzo ya koromeo) au saratani ya tezi.

***BBC.***

Makala

# Nchi kukopa kuna manufaa lukuki

**Na Hamisi Kibari**

HIVI karibuni, nilikutana na andiko kwenye kundi moja sogozi, mtu akilalamikia deni la taifa kupanda.

Alikuwa akizungumzia taarifa ya Beki Kuu (BoT) iliyoonesha kwamba Deni la Taifa kwa takwimu za Machi 2023 limeongezeka hadi kufikia Sh trilioni 94.8 kutokea Sh trilioni 87 kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.9

Mtu huyo akawa anahoji kwa nini nchi yetu inaendelea kukopa na kukopa huku akiwa na ile nadharia kwamba eti kuna siku nchi itapigwa mnada!

Nilijaribu kujibu, lakini nimeona ni vyema nitumie wasaa kutoa elimu kuhusu kwa nini tunakopa kwa Watanzania wenzangu kwani inaonekana wengi hawajui na wanapotoka au kupotosha dhana hii.

Mimi nilipata bahati ya kuhudhuria semina iliyojikita kwenye eneo hilo kwa hiyo angalau nina elimu kidogo.

Kimsingi, tangu awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi yetu hadi awamu hii ya sita, serikali imekuwa ikikopa kwa sababu ya uhitaji wa kufanya miradi yenye tija kwa wananchi na pia imekuwa ikifanya hivyo kwa sababuinakopesheka na inaaminika.

Katika semina niliyopata elimu maridhawa kuhusu deni la taifa, kwa bahati nzuri moja wa walimu wetu alikuwa Gavana wa sasa wa Benki Kuu, Emmanuel Tutuba ambaye wakati huo alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha.

Wanasemina tulijifunza kwamba hatua ya kukopa au kutokopa inaanza na nakisi inayotokana na bajeti ya taifa.

Kwamba ukishakuwa na nakisi unalazimika kukopa kwa ajili ya kufidia pengo hilo.

"Na kimsingi tunakopa kwa sababu sisi ni matajiri. Maskini hawezi kukopa.

Tunakopa pia kwa sababu tunaaminika. Unaona mashirika makubwa kama Benki ya Dunia yanatukopesha ni kwa sababu tunaaminika," anasema Tutuba.

Anasema pesa hukopwa katika maeneo matatu; kwa ajili ya kuunga mkono bajeti (general budget support), kukopa kwa ajili ya sekta ambayo wadau wanadhani kuna changamoto zinazopaswa kutatuliwa kama vile sekta ya afya na mikopo ambayo ni kwa ajili miradi ambayo wafadhili wenyewe huamua kuipelekea fedha zao.

Cha msingi, ndugu zangu Watanzania, kinachopaswa kuulizwa katika mikopo ni fedha zinakwenda kufanya nini na siyo kwa nini zimekopwa!

Kama ilivyo kwa mtu binafsi, mkopo unatakiwa uwe ni kwa ajili ya kuwekeza ama kufanya jambo muhimu la dharura na siyo kukopa kwa ajili ya kuolea mke mwingine, au kustarehe kwa mfano.

Kwa mantiki hiyo, mtu yeyote makini hukopa ili afanye mambo ya mendeleo leo huku akilipa taratibu kwa sababu thamani ya fedha zake leo haiwi sawa kadri muda unavyokwenda.

Gazeti moja lilimkariri Mchumi Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Profesa Aurelia Kamuzora akafafanua kwamba endapo uwekezaji mzuri unafanyika katika mikopo inayochukuliwa, uchumi wa nchiutaendelea kukua.

"Deni la Taifa linavyozidi kukua, ndio uchumi wa nchi unakua na nafasi ya kuongezeka inakuwepo pia kama fedha zinapokopwa zinawekwa vizuri kwa sababu mtaji wa kufanya miradi mbalimbali unakuwepo," ananukuliwa na gazeti hilo akisema.

Profesa anazidi kufafanua kwamba mzunguko wa fedha nchini unaongezeka kama fedha zinazokopwa zinaingia katika miradi.

Kwa wanaokumbuka, fedha zilizobatizwa za korona, Sh trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) ambazo zilitumika kujenga miradi mingi ikiwemo ya madarasa, zilisababisha mzunguko mkubwa sana wa fedha kwa wananchi.

"Unajua hata nchi zilizoendelea zinakopa kwa ajili ya kufanya miradi mbalimbali na kuongeza mzunguko wa fedha. Sioni shida ya deni kuongezeka kama zinatumika kwa tija na hazingii mifukoni mwa watu," anasema.

**Unajua hata nchi zilizoendelea zinakopa kwa ajili ya kufanya miradi mbalimbali na kuongeza mzunguko wa fedha. Sioni shida ya deni kuongezeka kama zinatumika kwa tija na hazingii**

Kimsingi, wananchi wanapaswa kuelewa kwamba Deni la Taifa, linahusisha fedha zinazokopwa na serikali na zile zinakopwa na sekta binafsi.

Ufafanuzi ni kwamba sekta binafsi inapokopa nje, deni hilo husajiliwa Benki Kuu na hata malipo yake yanafanywa kwa fedha za kigeni zilizopo nchini.

Kuna sababu nyingi za serikali kulitambua deni linalokopwa na sekta binafsi kwani mhusika anaweza akahamisha fedha nyingi kwa mkupuo na kuleta athari katika uchumi wa nchi na lazima pia ieleweke fedha hizo zinakwenda kufanya nini. Kwa hiyo ukisikia Deni la Taifa, basi ujue kwamba zimo pia fedha zilizokopwa na sekta binafsi.

Wanasemina pia tulijifunza kwamba ni deni la serikali linalohusisha pia mikopo ya ndani na mikopo kutoka nchi au taasisi za kimataifa. Mikopo ya ndani ni ile inayohusisha hati fungani. Kwa hiyo, hiyo pia ujumuishe kwenye Deni la Taifa.

Yaani badala ya wananchi kuweka fedha kwenye baadhi ya mabenki kwa akaunti ya muda maalumu, kupitia hati fungani wananchi hupata faida kubwa na hivyo kuboresha zaidi uchumi na maisha yao.

Wananchi wanapaswa kujua pia kwamba mikopo mingi ambayo nchi imekopa iko katika masharti nafuu ambayo riba yake ni chini ya asilimia moja na kipindi cha kuiva mikopo hiyo ni hadi miaka 40.

Hata hivyo, kuna mikopo iliyo katika masharti ya kati ambayo riba yake ni chini ya asilimia 3 na kipindi cha kuiva mkopo ni hadi miaka 15 mpaka 20.

Kadhalika kuna mikopo michache sana ambayo nchi imekopa ikiwa katika masharti ya kibiashara ambayo riba yake inalingana na hali ya soko na kipindi cha kuiva ni miaka saba.

Wanasemina tulijifunza kwamba sababu ya kuwepo kwa haja ya kukopa ni pamoja na ongezeko la watu na mahitaji yao, mapato ya ndani kutokidhi mahitaji ya vipaumbele vilivyopo na haja ya kufungua miundombinu ya mitaji ilikuongeza pato la mtu mmoja mmoja.

Sababu nyingine ni kuongeza mapato ya ndani kwa kufungua miradi inayozalisha zaidi na kuzuia mtikisiko wa thamani ya shilingi.

Lakini pia sababu nyingine ni tabia za mkopaji kwamba tunakopa kwa mahitaji sahihi, uwezo wa kulipa, dhamana na kuangalia masharti ya mikopo.

Wanasemina ambao wengi tulihakikishiwa pia kwamba mpaka sasa deni la taifa ni himilivu.

"Maana ya deni kuwa himilivu ni endapo serikali itakopa ina uwezo wa kulipa madeni yake ya sasa na madeni yake yatakayoiva baadaye bila kuathiri ukuaji wa uchumi na shughuli nyingine za serikali ikiwemo kutoomba msaada wa kulipa madeni kutoka mataifa au taasisi nyingine," anasema mmoja wa watoa mada kwenye semina hiyo.

Anasema kwa sasa Tanzania ni nchi inayokimbiliwa na wakopeshaji kulingana uhimilivu wake.

Cha msingi elewa ndugu Mtanzania mwenzangu kwamba, kama si kukopa baadhi ya miradi ingechukua hata miaka 70 kukamilika kama ni kutegemea makusanyo ya fedha za ndani lakini miradi hiyo zikiwemo barabara tunandelea kutumia huku tukilipa kidogo kidogo.



Gavana wa Benki Kuu Tanzania, Emmanuel Tutuba



Na Hamisi Kibari
Mtanzania wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 9

**Chris anahamia nyumbani kwake na hawara yake Joyce ili kupunguza gharama za kuishi hoteli baada ya mkewe kwenda nyumbani kwao kutokana na manyanyaso ya mumewe. Mkewe anaporejea ghafla kunatokea mtafaruku baina ya mkewe huyo na hawara, hali inayosababisha mfanyabiashara huyo anayeendesha duka kubwa la mbao na vifaa vya ujenzi ampige mkewe hadi kuzirai. Chris analazimika kumpeleka hospitali mkewe akiwa hajitambui na kuwadanganya ndugu wa mkewe kwamba alitoweka na kwenda kusikojulikana. Daktari aliyekuwa akimtibu anamjulisha kwamba mkewe amefariki dunia. Daktari huyo anampa njia itakayosaidia asishitakiwe kwa mauaji. Chris anakubali njia hiyo lakini gharama za kuficha kifo hicho ni kubwa. Ndugu wameanza kumtafuta mke wa Chris. Nini kitatokea? Endeleeni.**

Mama Kessy ambaye alikuwa ameketi kwenye stuli kumsikiliza mgeni wake huku povu la sabuni halijakauka kwenye mikono yake alibaki ameduwaa. Jacob akendelea kuongea wakati Mwalimu Misango akitafakari.

“Unajua mwalimu, yule mdogo wangu ninamfahamu. Ana roho nyepesi. Wakati fulani kama nilivyowahi kusema alikorofishana na shangazi akatishia kunywa sumu ili kujitoa uhai. Tendo la kuletewa hawara ndani, tena chumbani mwake, anaweza kabisa kujinyonga.””Hilo mimi silifikiri sana kwanza tungeshapata habari tangu alipotoweka toka majuzi. Leo siku ya tano, siyo? Tungeshasikia redioni au kusoma magazetini. Lakini suala la polisi sasa ni muhimu.””Mwalimu, siyo kila tukio linaripotiwa polisi. Mbona kuna jirani yetu pale alimuua mke wake kwa shoka lakini hadi leo sijawahi kusikia redioni wala wapi? Pia anaweza akawa kafia machakani au maiti yake ikiwa bado iko chumba cha maiti hospitalini ikiwa haijatambuliwa.””Acha kumwazia hayo wifi yangu mpendwa, Jacob.””Mimi ninakuomba, usitishe kufua, tuongozane hadi polisi kutoa taarifa, na baadaye ninafikiri twende kumsaka mahospitalini.””Kwa nini tusimpe Chris siku ya leo tena ya kumtafuta mkewe?” “Sidhani kama ni busara kuendelea kukaa kimya bila kumtafuta. Hata polisi watashangaa leo siku ya tano, mtu haonekani halafu hatujapeleka taarifa yoyote polisi.””Lakini kumbuka jioni tutakuwa na kikao nyumbani kwake. Unaonaje tulizungumzie hilo wakati huo?””Sisi kama watu wazima lazima tujaribu kuchukua hatua haraka badala ya kujibweteka tu, mwalimu.” “Mdogo wako bado ni binti mdogo na mrembo sana. Anaweza kuwa kaamua kuchukua bwana ili amkomoe mdogo wangu kutokana kumletea mwanamke ndani. Aliwahi kunitamkia hilo kwamba bwanamdogo asifikiri kwamba yeye hakuna wanaume wanaomtafuta usiku na mchana lakini analinda heshima ya ndoa yake. Hata mara ya mwisho nilipoongea naye kwa simu baada ya kutoweka nyumbani alisema haoni kama kuna ndoa tena na eti anajiandaa maisha ya kivyakevyake na akipata bwana hatosikiliza la mtu. Kuna wakati ninawaza hilo pia kwa sababu asingeweza kuondoka nyumbani bila kuja hapa kwangu ama kwako kama ulivyosema.””Una hakika ulimsikia Mama Kenny akitamka maneno hayo?”

“Tena si mara moja. Alisema kama si mapenzi kwa watoto wake na heshima anayoendelea kumpa mumewe angashajikabidhi kwa mwanaume mwingine kitambo.””Hilo pia linawezekana, lakini kadri ninavyojua dada hana tabia ya aina hiyo. Ni mtu aliyempenda kwa dhati mumewe na kuheshimu ndoa yake... Ndio maana naomba, hata kama hilo la kusaka mwanaume kulipiza kisasi linawezekana pia lakini lisituzuie kwenda kutoa taarifa polisi kwamba Tausi hajulikani alipo. Nadhani hiki ndicho kinatakiwa kufanyika sasa.”

“Leo Jumapili, sina hakika kama tutapata huduma nzuri polisi. Naomba tutoe taarifa kesho. Sasa hivi kama unavyoona bado ninafanya udobi.”

“Unajua kinachonisumbua ni kile nilichohofu kwamba isije ikawa kajinyonga. Yule roho yake nyepesi anapokuwa na matatizo na ndio maana alifikia kukwambia kwamba anaweza naye kulipa kisasi kwa kutoka nje ya ndoa. Unadhani, Mwalimu,mtu mwenye subira anapokumbwa na matatizo anaweza kusema maneno kama hayo?”Mama Kessy aliangalia chini, na kukuna kichwa.* * *Dk. Nimrod Goima na Chris waliketi katika pembe moja ya hoteli ya Lemon Tree wakinywa na kula nyama choma. Kama kawaida, Chris alikuwa akinywa bia na Dk. Goima akinywa soda.Daktari alikunywa mikupuo miwili ya soda kisha akamgeukia Chris: “Sikiliza Bw. Magati. Tumewaita watu wa Halmashauri ya Mji kuja kuzika maiti za watu wasio na ndugu ambazo zimeshakaa kwenye chumba cha kuhifadhia maiti zaidi ya wiki mbili. Ingawa maiti ya mkeo haijafikisha siku hizo lakini nina uhakika kesho itazikwa.””Itakuwa vizuri sana.””Pamoja na advance ya Sh milioni 20 ulizotoa, lakini kuficha kifo cha mkeo ni jambo linalowahusisha watu wengi ili kulifanikisha, kwanza watu wa chumba cha maiti, watu wa ‘records’ pale hospitalini na wauguzi wa wodi ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu alikokuwa amelazwa. Tayari jina la mkeo, limeshaondolewa kila mahala na anaorodheshwa kama mgonjwa ambaye hajulikani, yaani unknown patient. Hawa wote wanasubiri mgao. Jitahidi kesho kabla maiti ya mkeo haijaenda kuzikwa niwape watu mgao wao wasije wakatibua mambo.””Kwa kesho itakuwa ngumu kwa sababu ninaendelea ku-process mkopo,” alisema Chris.”Itakuwa ngumu Mr Magati. Kumbuka nilikuondolea milioni 10 kutoka 50. Hawa watu hawawezi kunielewa,” alisema Dk. Goima.

“Dokta, ninaomba unisaidie. Leo nitaongea na meneja wa benki na hivyo ninahitaji siku chache tu. Almost wiki.””Hata hapo nimekusaidia sana na kwakweli ninahatarisha sana kibarua changu. Usiku kucha nilikuwa ninawaza hili. Yaani hapa ninachezea Shilingi kwenye tundu la sindano. Fanya juu chini hii pesa ipatikane.””Kuna gari langu liko gereji huu mwezi wa tatu nasubiri spare kutoka Japan, kesho nitakuletea kadi ya gari kama dhamana.”

“Hilo gari lina thamani ya Sh milioni 20. Ni aina gani na mwaka gani?”

“Linakaribia hiyo thamani, Isuzu trooper, new model.”

“Hapana. Labda kama utanipa hati ya nyumba au kiwanja ambacho kiko prime area.””Dokta. Naomba uwe mtu mwenye subira. Hakuna njia ya mkato katika hili. Kama umeamua kunisaidia endelea kunisaidia. Kwanza kwa kiasi nilichotoa almost nimechukua working capital yote ya biashara zangu. Nimefanya hivyo ili ku-rescue hii situation kwa sababu pesa hutafutwa lakini nikiswekwa ndani nitazitafutia wapi?”* * *Huku Mwalimu Misango akiwa amesimama pembeni mwake Jacob aliendelea kutoa maelezo ya kutoweka kwa dada yake, hiyo ikiwa imeingia siku ya sita.

**Dokta. Naomba uwe mtu mwenye subira. Hakuna njia ya mkato katika hili. Kama umeamua kunisaidia endelea kunisaidia. Kwanza kwa kiasi nilichotoa almost nimechukua working capital yote ya biashara zangu. Nimefanya hivyo ili ku-rescue hii situation kwa sababu pesa hutafutwa lakini nikiswekwa ndani nitazitafutia wapi?**

“Umesema wewe ni kaka yake, siyo?” Alihoji askari aliyekuwa akiandika maelezo.

“Ndiyo.”

“Mmezaliwa tumbo moja?”

“Hapana. Ni mtoto wa baba yangu mdogo aliyenisomesha. Baba alipofariki dunia nikiwa mdogo sana, baba mdogo akanichukua kwa hiyo nimekulia kwao.”

“Umri wake?”

“Miaka 27.”

“Alishawahi kuolewa?”

“Ndiyo na ana watoto wawili.”

“Aliachika kwenye ndoa?”

“Hapana. Bado yuko kwenye ndoa?”

“Mume wake amesafiri.”

“Hapana, yupo.”

“Yupo hapa Tabora?”

“Ndiyo.”

“Kwa nini hamjaambatana naye? Kwa sababu mume ana nafasi nzuri kulisaidia Jeshi la Polisi kuliko wewe kaka. Maswali ambayo ningemuuliza, wewe siwezi kukuuliza.”

Swali lilionekana gumu kidogo kwa Jacob. Wakati akijitafuta namna ya kulijibu, Mwalimu Misango aliingilia kati.

“Yeye bado anamtafuta mkewe. Ndiye ametutuma.”

“Na wewe ni nani?”

“Mimi ni wifi yake. Yaani huyo mume wake uliyekuwa unamuulizia, ni mdogo wangu.”

“Asante Mwalimu Misango. Habari za siku nyingi?”

“Nzuri... Tunafahamiana.”

“Ulinifundisha. Nadhani nilikuwa darasa la sita wakati unakuja shuleni kwetu na kama sikosei ndio ulikuwa unaanza kazi. Miaka imepita. Huwezi kunikumbuka.”Baada ya kutoka kwenye kaunta ya kituo cha Polisi, Yakobo alimgeukia Mama Kessy: “Mimi ninashauri sasa twende hospitali tukamtazame mawodini na mochwari. “Lakini polisi wamesema kama wifi angekuwa na tatizo lolote angekuwa na taarifa... Pengine si vibaya tukienda sasa hivi lakini ninashauri twende kesho. Unaonaje?””Mwalimu, ingefaa twende leo. Nitachukua teksi ituzungushe,” alijibu Jakob.”Ninaomba unisamehe, Jacob ninatakiwa ofisini. Nilikudokeza kwamba mimi ndiye mwalimu wa zamu wiki hii.

***Itaendelea.***



## Israel yamrejesha nyumbani Balozi wake A. Kusini

**YERUSALEM, Israel**

ISRAEL imemrudisha nyumbani Balozi wake wa Afrika Kusini, Eliav Belotserkovsky, kwa mashauriano, Waziri wa Mambo ya Nje wa Israel, Lior Haiat, amesema kupitia X bila kutoa maelezo zaidi.

Afrika Kusini imekuwa ikikosoa vikali operesheni ya kijeshi ya Israel huko Gaza.

Siku ya Jumatatu iliitaka Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC), kutoa hati ya kukamatwa kwa Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu, kabla ya kufika katikati ya Desemba, mwaka huu.

Kuondolewa kwa Balozi wa Israel, Belotserkovsky, kunakuja muda mfupi kabla ya Afrika Kusini kuwa mwenyeji wa mkutano kuhusu vita vya Israel na Hamas wa kundi la mataifa ya Brics, linalojumuisha China na Urusi.

Pia siku ya Jumanne, Bunge la Afrika Kusini, linatarajiwa kupiga kura kuhusu kufunga ubalozi wa Israel na kusimamisha uhusiano wote wa kidiplomasia hadi Israel itakapokubali kusitisha mapigano na kukubali kufanya mazungumzo yatakayo simamiwa na Umoja wa Mataifa.

# Mackenzie, wenzake kuendelea kushikiliwa



**NAIROBI, Kenya**

MCHUNGAJI mwenye utata ambaye pia ni mshukiwa mkuu wa mauaji ya Shakahola, Paul Mackenzie, ataendelea kushikiliwa hadi Desemba 22, mwaka huu mahakama itakapotoa uamuzi kuhusu ombi lililowasilishwa na upande wa mashitaka kutaka kumweka kizuizini yeye na mwenzake kwa miezi sita zaidi.

Akifikishwa mahakamani, Mkurugenzi Msaidizi wa Mashitaka ya Umma, Jami Yamina, alielezea hofu kwamba washtakiwa wanaweza kujiua ikiwa wataachiliwa.

Muda wa nyongeza, alisema utaruhusu polisi kukamilisha uchunguzi kuhusu suala hilo.

Wakati ukitoa kesi yake, upande wa mashitaka ulidai kuwa Katiba inaruhusu kuzuiliwa kwa washukiwa wa ugaidi kwa hadi siku 360.

Mkurugenzi Msaidizi wa Mashtaka ya Umma alisema kuwa Bunge pia limeidhinisha uamuzi wa kuongeza muda wa kuwekwa kizuizini kutoka siku 90 hadi siku 360 katika kesi tata.

Yamina katika hoja yake pia alipinga uamuzi wa mahakama wa kuwaachilia washukiwa sita kati ya 29 kulingana na mapendekezo yaliyotolewa na Idara ya Huduma za baadaye.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Msaidizi wa Mashitaka ya Umma, washukiwa hao watahitaji kufanyiwa mpango wa kuondokana na msimamo mkali, ikimaanisha kuwa watahitaji kufundishwa jinsi ya kuyakabili maisha kwa njia tofauti.

Kwa mujibu wa Yamina, mpango huo utawasaidia kabla ya kuunganishwa tena katika jamii.

Mackenzie anakabiliwa na mashitaka ya ugaidi kutokana na mauaji ya zaidi ya watu 300 kupitia madhehebu aliyoyaongoza kwa mahubiri ya upotoshaji.

Mchungaji huyo mara kadhaa amenyimwa dhamana na anaendelea kuzuiliwa na mamlaka.

# Korea Kaskazini kurusha satelaiti ya kijasusi



**PYONGYANG, KOREA KASKAZINI**

KOREA Kaskazini ilisema huenda ikajaribu kurusha satelaiti ya tatu ya kijasusi mapema usiku wa kuamkia leo Jumatano, vyombo vya habari vya Japan vimeripoti.

Tokyo ilisema Pyongyang imewajulisha kipindi cha siku tisa cha uzinduzi huo, kitakachofungwa saa 23:59 saa za eneo (14:59 GMT) Novemba 30, mwaka huu.

Japan itashirikiana na Korea Kusini kuhimiza vikali Kaskazini kutoendelea na uzinduzi huo, ambao walisema utakiuka maazimio ya Umoja wa Mataifa.

Pyongyang imeshindwa mara mbili mwaka huu kurusha satelaiti ya kijasusi angani.

Walinzi wa Pwani ya Japan, walisema arifa ya Pyongyang ilitenga maeneo matatu ya baharini yanayoaminika kuwa maeneo ambayo vifusi vya roketi iliyobeba satelaiti hiyo vitaanguka.

Mawili yako magharibi mwa rasi ya Korea na jingine liko mashariki mwa kisiwa cha Luzon cha Ufilipino.

Kang Ho-pil, Mkurugenzi Mkuu wa Operesheni katika Wakuu wa Pamoja wa Wafanyakazi wa Korea Kusini, alionya kwamba Seoul itachukua hatua stahiki ikiwa uzinduzi utaendelea.

Satelaiti ya kijasusi ni kama tunu inayotamaniwa kwa kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un, kwani itamruhusu kufuatilia mashambulizi yanayokuja na kupanga njama yake kwa usahihi zaidi.

Hata hivyo, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limepiga marufuku Pyongyang kurusha satelaiti kwa sababu inaziona kama kisingizio cha kujaribu teknolojia ya makombora ya Kaskazini.

BBC.

# Israel yauzingira mji wa Gaza



**YERUSALEM, Israel**

JESHI la Israel limesema kuwa limeuzingira mji wa kaskazini wa Gaza wa Jabalia huku likisema vikosi vyake viko tayari kwa awamu inayofuata ya vita.

Jabalia iko kaskazini mwa Jiji la Gaza ambalo limeshuhudia mapigano makali zaidi ya vita.

Katika taarifa jana, Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF), lilisema limefanya mashambulizi kwenye maeneo 250 ya Hamas katika siku ya mwisho kwa kutumia ndege za kivita na ndege za mbali.

Hii ilijumuisha mahandaki matatu katika eneo la Jabalia na kuua makumi ya wapiganaji, IDF iliongeza.

Hata hivyo, BBC haiwezi kuthibitisha mara moja madai mengi katika uwanja wa vita. BBC.

## ABDALLAH GAMA:

# Atimiza miaka 67 na tawasifu nzito ya muziki wa dansi

■ **Ni gwiji wa kucharaza gitaa aliyetamba Sikinde, Bima Lee na nje ya nchi**



Wanamuziki wa Bendi ya Mlimani Park (kutoka kushoto) Julias Mzeru, Fresh Jumbe, Cosmas Chidumule na Henry Mkanyia wakifanya mazoezi ya nyimbo mpya siku chache baada ya Gama na wenzake kuhamia Bima.

**Na Hamid Yassin**

HIVI karibuni mwanamuziki nguli katika medani ya muziki dansi nchini, Abdallah Ally Gama 'String Master' ametimiza miaka 67 ya kuzaliwa na kuandaliwa hafla kamambe na familia sambamba na wadau mbalimbali wa muziki wa dansi.

Ingawa hivi sasa ni nadra kumkuta Gama kwenye majukwaa ya bendi za muziki, lakini hiyo haikuwazuia wadau hao kumwandalia hafla hiyo iliyofanyika nyumbani kwao Temeke Dar es Salaam.

Nguli huyu ni mmoja miongoni mwa wanamuziki 12 ambao mwaka 1978 walijiengua kwenye kundi la Dar International kwa madai ya kupinga uongozi mbovu wa mmiliki wao, Zachariah Ndabameiye na kuanzisha bendi ya Mlimani Park Orchestra.

Waliondoka kwa madai ya kupinga uongozi mbovu wa mmiliki wao, ambapo imeelezwa kuwa baada ya kujiengua walikwenda kuungana na wanamuziki wengine akina Abel Bartazal, George Kessy, Haruna Liwali na Ibrahim Mwinchande (wote hawa wameshatangulia mbele ya haki) na kuwa waanzilishi wa bendi ya Mlimani Park Orchestra.

Baadhi ya wanamuziki wengine waliochomoka Dar International na kwenda kuanzisha bendi hiyo walikuwa ni marehemu Michael Enock, aliyekuwa mtaalamu wa kupiga ala zote za muziki, Cosmas Chidumule, marehemu Joseph Mulenga 'King Spoiler', marehemu Machaku Salum, marehemu Joseph Benard na Habib Jeff.

Wakati akiwa kwenye bendi ya Dar International aliyoitumikia kuanzia mwaka 1977, Gama alishiriki kupiga Rhythm kwenye vibao vingi, baadhi yake vikiwa ni 'Sikitiko', 'Mwana Rudi Uoe' na 'Mwalimu Nyerere'.

Alipoingia katika bendi hiyo ya Mlimani Park Orchestra, Gama kwa kipindi kifupi aliweza kujipatia umaarufu mkubwa, hasa kwa umahiri alioonyesha katika kulicharaza ipasavyo gitaa la Rhythm kwenye vibao vingi vya bendi hiyo.

Pia Gama ni mwanamuziki aliyefaulu kwa kiasi kikubwa kuzigusa nyoyo za mashabiki wengi kutokana na tungo zake zenye maudhui maridhawa yaliyoshiba ujumbe mzito, za 'Hadija', 'Chenga ya mwili Dar es Salaam Airport', 'Maudhi ya Nyumbani', 'Linda' na 'Nawashukuru Wazazi'.

Mbali ya kutunga, Gama alipiga gitaa hilo la rhythm na chache la solo katika nyimbo nyingi za Sikinde Ngoma ya Ukae zilizotungwa na wanamuziki mbalimbali waliopitia bendi hiyo tangu kuasisiwa kwake.

Akielezea wasifu wake katika hafla hiyo ya kuzaliwa kwake, Gama alianika mambo mengi hususani historia ya kimuziki na maisha yake kwa ujumla.

"Baba yangu alikuwa fundi Cherahani, ndiye aliyenivuta kwenye muziki kwani alikuwa akipiga gitaa lisilotumia umeme la Galatoni, kujifurahisha na wakati mwingine akiwaburudisha rafiki zake," anasema Gama.



Alisema kuwa, akiwa na umri wa miaka 18, alikuwa tayari anafahamu kikamilifu jinsi ya kulikung'uta gitaa. Bendi yake ya kwanza kupigia ilikuwa ni Safari Trippers aliyojiunga nayo mwaka 1973.

"Nikiwa Safari Trippers nilishiriki kupiga gitaa la solo kwenye vibao kadhaa, vikiwamo 'Ooh Lila' na 'Mateso' ambavyo vyote ni matunda ya marehemu Marijani Rajabu," alibainsha Abdallah Gama.

Ni mwanamuziki asiyependezwa na tabia ya wanamuziki kuhamahama makundi, alisema kwamba mwaka 1975 alijiunga na bendi ya Tanzania Stars ambayo maskani yake yalikuwa katika hoteli ya Margot.

Hoteli hiyo ilikuwa katika mtaa wa Independence (siku hizi ni mtaa wa Samora) jijini Dar es Salaam. Ikumbukwe kuwa, mwaka 1984 Gama alijiunga bendi ya Bima Lee iliyokuwa ikimilikiwa na Shirika la Bima la Taifa (NIC).

"Nikiwa na bendi ya Bima Lee, iliyokuwa ikipiga muziki kwa mtindo wa 'Magnet Tingisha', nilitunga kibao cha 'Fungua Macho', pamoja na kushiriki kucharaza gitaa kwenye vibao kama vile; 'Makulata'

'Fanya kazi', 'Linalonisubu moyo', 'Tujemazo', sambamba na kufanya kufuru kubwa katika wimbo wa 'Frocy' ambao nilirindimisha gitaa la rhythm vilivyo," anafafanua Gama.

Gama atakumbukwa kwa kazi zake alipokuwa bendi ya Bima Lee Orchestra akishirikiana vyema na watunzi na waimbaji akina marehemu Jerry Nashon, marehemu Shaaban Dede, wapiga magitaa marehemu Joseph Mulenga 'King Spoiler' kwa upande wa solo na marehemu Suleiman Mwanyiro 'Compyuta' kwa upande wa gitaa zito la besi.

Wanamuziki hao walichukuliwa kwa mpigo na Shirika hilo la Bima kutoka bendi ya DDC Mlimani Park kwa ajili ya kuimarisha bendi ya Bima Lee Orchestra kufuatia ushindani mkubwa wa bendi zilizokuwepo wakati huo.

Gama wakati huo alikuwa mithili ya Kito cha thamani kwani aliitumikia bendi ya Bima Lee Orchestra kwa mwaka mmoja.



Abdallah Gama

>>>Inaendelea Uk. 21

# Atimiza miaka 67 na tawasifu nzito ya muziki wa dansi

>>>Inatoka Uk. 20

Mwishoni mwa mwaka 1985, alihitajika kurejea tena katika bendi yake ya zamani ya Sikinde.

Wimbo wa 'Gama Unisamehe' ni kibao kilichoporomoshwa na bendi yake wakati huo ya Mlimani Park Orchestra, baadhi ya wapenzi na mashabiki hudhani kwamba mtunzi wa wimbo huo kuwa alikuwa yeye, lakini Gama pasipo kujigamba ametamka kwamba;

"Kibao kile kilitungwa na Tshimanga Kalala Asossa, tukiwa Zanzibar kwenye shoo, mimi nilikuwa Kiongozi wa Jukwaa, sasa kabla hatujaanza kutumbuiza nilipanda jukwaani na kuwaita wanamuziki kwa kutumia mlio maalum wa gitaa langu...," alibainisha.

Nguli huyo aliendelea kueleza kuwa, ghafla alimuona Asossa aliyekuwa anapenda kutembea na redio ndogo ya kurekodia sauti, akarekodi kipande alichokuwa anakipiga kisha akaondoka.


Waliporejea Dar es Salaam wakiwa kwenye mazoezi, Tshimanga Kalala Asossa alikuja na mashairi ya wimbo huo, akiambatanisha kilekipande alichokipiga Gama kule Zanzibar.

Wakaufanyia kazi wimbo huo na kuamua kuupa kumbukumbu kwa kuuita 'Gama Unisamehe'. Tshimanga Asossa alijiunga na bendi hiyo ya Mlimani Park Orchestra mwaka 1981, baada ya uongozi wa Mlimani Park kumfuata kwao Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), kuja kupiga muziki na bendi hiyo kwa mkataba.

Maisha ni kutafuta usemi huo ulijionesha wazi kwa mwanamuziki Abdallah Gama, ambaye mwishoni mwa mwaka 1985, alivuka mpaka wa Tanzania na kuingia nchini Kenya kwa kupitia bandari ya Tanga.

Alipotua katika Jiji la Nairobi, alijiunga na bendi ya Super Mazembe iliyokuwa ikitumbuiza kwenye ukumbi wa Garden Square, jijini Nairobi. Alishirikiana kikamilifu na wapiga magitaa wa bendi hiyo ya Super Mazembe akina Loboko Bua Mangala, Bukasa wa bukasa Bukalos, Atia Joe Mwanza wa Mwanza aliyekuwa akilingurumisha gitaa la besi.

Matarajio ya kila kazi ni kupata




**Aidha, anazikumbuka baadhi ya nchi alizowahi kufika kuwa ni pamoja na Japan, Malaysia, Ufilipino, Pakistan na Misri. Bila kusita Gama amesema kuwa yeye ni baba wa watoto wanne anawataja kuwa ni Mgeni, Pili, Hadija na Maimuna. Elimu kwa familia yake aliipa kipa umbele na sasa anajivunia kwa kuweza kusomesha watoto wake...**

mafanikio mazuri yanayoweza kumnemesha muhusika pamoja na familia yake.

Kwa upande wa mafanikio aliyoyapata mwanamuziki huyo, anasema kuwa, ni pamoja na kutembea nchi nyingi duniani, jambo ambalo hakutarajia hapo kabla. Kati ya ziara alizowahi kufanya nje ya nchi, anaikumbuka mno ziara yake alipokuwa katika bendi ya Malembe Stars.

Aidha, anazikumbuka baadhi ya nchi alizowahi kufika kuwa ni pamoja na Japan, Malaysia, Ufilipino, Pakistan na Misri. Bila kusita Gama amesema kuwa yeye ni baba wa watoto wanne anawataja kuwa ni Mgeni, Pili, Hadija na Maimuna. Elimu kwa familia yake aliipa kipa umbele na sasa anajivunia kwa kuweza kusomesha watoto wake wote hadi elimu ya Chuo Kikuu.

Ili kutunza kumbukumbu za kazi zake alizokwisha kuzifanya awali, Gama ana mpango wa kurudia kuvirekodi upya vibao vyake vya zamani, alivyovitunga akiwa na bendi za Mlimani Park Orchestra Wana Sikinde na Bima Lee Orchestra, kutokana na shinikizo kubwa la mashabiki wake.



Abdallah Gama alivyo sasa.

Gama miaka ya hivi karibuni aliwahi kupewa jukumu la kuisuka bendi ya Excel ya jijini Dar es Salaam, wakati akiwa katika mkakati wa kuanzisha bendi yake binafsi jitihada ambazo hata hivyo hakufanikiwa na kuishia katika tatizo la ulevi wa kukithiri hadi pale wanafamilia kwa kushirikiana na wadau wengine wa muziki wa dansi walipoamua kumvalia njuga kumuondosha katika tatizo hilo la ulevi na kumpa ushirikiano wa kumjenga kisaikolojia.

Hatua ya kufanyiwa 'birthday' ni katika jitihada hizo za kumjenga upya kisaikolojia ili aweze kurudi katika mchango wake wa kisanaa katika muziki hata kwa ushauri kama zamani ikizingatiwa bado ana uwezo mkubwa wa kumbukumbu za matukio muhimu ya kimuziki.

**Maoni; 0768 888 787.**




# Je, tuna ujasiri wa kuhoji uhalali wa namba tatu ya IFFHS ya Yanga barani Afrika?

**Na Ibrahim Mkamba**

KWA mujibu wa utafiti wa mtandao wa IFFHS, Yanga ni timu ya tatu kwa ubora Afrika nyuma ya Al Ahly ya Misri na Wydad AC ya Morocco. Naamini takwimu hizo hazina utata wowote na hayo ni matunda ya Yanga ya upambanaji wao wa kipekee uwanjani.

Akitokea mtu wa kuchukia matokeo ya utafiti huo, mtu huyo atakuwa anachukia fighting spirit (ari ya upambanaji) ya Yanga.

Uhalali wa kuhoji takwimu za IFFHS zilizoiweka Yanga namba tatu Afrika umepotea baada ya Yanga kuwemo ndani ya tano bora ya kugombea timu bora ya Afrika ya 2022/2023. Walikuwa 10, watano wamechujwa kuondolewa na watano wamebaki, Yanga ikiwemo katika hao watano waliobaki.

Yaani kutoka timu zaidi ya 60 za kueleweka za bara hili, zikabaki tano bora, ukiwemo, wewe ni mshindi hata usiopokuwa namba moja.

Hebu tuwekane sawa hapa. Kihalali kabisa timu inapanda juu kimafanikio kwa kucheza robo fainali nyingi ligi ya mabingwa Afrika. Hapo huwa wanakuwa ndani ya timu nane bora za bara hili kwenye mashindano hayo makubwa. Sasa Yanga wamo ndani ya tano bora na lolote linaweza kutokea.

Ukweli Yanga wanastahili kila shavu linalohusu uchezaji.

Ukiwatazama wachezaji wa Yanga wakicheza, utadhani nao ni wamiliki wa klabu ya Young Africans. Wanacheza si kama waajiriwa bali kama wenye mali! Hili kwa hapa kwetu halipo kwenye timu yoyote nyingine.Jana nilitazama kwa kutulia kupitia Azam Tv mechi yao ya ligi kuu na Singida Big Stars na kushangaa ilikuwaje mechi hiyo ikamalizika kwa Yanga kushinda 2-0 tu! Moto waliokuwa wakipelekewa SBS ulikuwa wa ukali wa kutisha.

Yanga sasa hivi wanafanikiwa kwa kuwa na uongozi imara wa mikakati mingi sahihi,

> **Jambo jingine ambalo Yanga imezizidi timu nyingine tangu enzi na enzi ni kumfanya kila mchezaji...**

upendo na maelewano ya wote kuanzia wachezaji, viongozi, wanachama, mashabiki na kila mtu. Ukiona mashabiki wa Yanga wanamzomea mchezaji na kumtupia chupa za maji mchezaji (jambo baya lisilokubalika) basi mchezaji huyo ni wa timu pinzani na si wa Yanga.

Yanga walifungwa na timu ndogo ya Ihefu 2-1 lakini hakukuwa na wachezaji wa Yanga waliosemwa vibaya na mashabiki wa Yanga na wala haikutumika nguvu yoyote kuwashawishi mashabiki wao kuhudhuria tena kwa wingi viwanjani baada ya kipigo hicho cha kushtukiza (sucker punch). Zingatia walishindwa mechi hiyo kabla wapinzani wao wa karibu Simba wakiwa hawajashindwa wala kupata sare mechi yoyote, wakishinda mfululizo mechi zao.

Pia Yanga wamejenga utamaduni wa kuheshimu mipaka ya kazi. Hakuna shabiki wa Yanga aliyewahi kuhoji kwa nini Farid Mussa, Kibwana Shomari na Salum Abubakar hawachezi. Kuheshimu huko mipaka ya majukumu kunafanya kila mtu atimize wajibu wake kwa kujiamini.

Jambo jingine ambalo Yanga imezizidi timu nyingine tangu enzi na enzi ni kumfanya kila mchezaji anayeichezea Yanga, Mtanzania na asiye Mtanzania, kuifanya Yanga kuwa kitu muhimu mno kwa maisha yake hata kama utotoni mchezaji huyo hakuwa shabiki wa Yanga.

Hii ndiyo inayosababisha upambanaji mkubwa kwani wachezaji wa Yanga hutanguliza kuipenda timu hiyo mbele ya kitu chochote. Kuthibitisha hilo, wachezaji wa zamani wa Yanga huwa karibu mno na Yanga tofauti na wa zamani wa timu nyingine. Hao wa timu nyingine wakishatoka, utawatafuta.

Nimalize kwa kusisitiza kuwa Yanga iko juu Afrika na itazidi kwenda juu kutokana na mipango yake mizuri na upendo ulioenea miongoni mwa wanaoihusu timu hiyo. Ni wakati wao sasa kufikiria makubwa na kujipanga kwa makubwa.






## Kona ya Urembo

Na Hidaya Machuppa
Simu: +255 765 828 219

# Kitenge vazi la linalotamba wakati wote









UVAAJI wa mwafrika unabadilika kila siku kama nchi za Magharibi zinavyobadilisha mitindo yao. Wiki hii tunazungumzia ubadilikaji wa uvaaji wa mwanamke au mwanaume wa kiafrika.

Kutokana na wingi kwa mikato na aina ya vitambaa vya kiafrika tumekuwa na sisi tukionekana wapya kila siku kutokana na mchanganuo wa mitindo na kuibuka kwa wabunifu chipukizi kila siku.

Tukiachilia wingi wa vitambaa vinavyopatikana Afrika sisi watanzania pia tunajivua kanga, kaniki, vitenge, bazee na aina nyinginezo nyingi za vitambaa.

Nimeona tumuongelee umaridadi unaotokana na kitenge ambacho ndo kitambaa chenye umaarufu mwingi kwa Africa na Kila nchi inatengeneza kitenge hivi sasa mpaka bara la Asia nchi kama china sasa inatengeneza vitenge. Hii ni kutokana na kuwa na soko kubwa.

Hivi hujioni wa ajabu unapokuwa huna kitenge au vazi lililotengenezwa kwa kitenge ndani ya kabati lako? Nimegundua swala kubwa si ukosekanaji wa kitenge ila ubunifu katika uvaaji wa kitenge.

Mambo makuu ya kuzingatia katika kutengeneza vazi la Kitenge.

1. Angalia mpangilio wa maua kama ni rahisi katika kushoneka na ikakaa vizuri, sio kila kitenge ni cha kushonwa vingine vimebuniwa kwa ajili ya kuvaliwa kwa mfumo wa kufungwa.

2. Zingatia rangi. Kila ngozi ya binadamu inaendana na rangi fulani ya mavazi, usivae tu kitenge kwakuwa mwenzio amevaa, ila vaa kitenge kwakuwa kinaenda na rangi yako.

3. Umbo la mwili wako pia linachangia kupendeza kutokana na aina ya mshono utakaoshona.

Angalizo: gauni ndefu za kitenge zinapendeza watu wa kila umbo. Usijibane na kushindwa kupendeza.





# Pellegrino aitaka Taifa Stars

NYOTA wa kimataifa wa Tanzania anayekipiga nchini Norway, Amahl William Pellegrino amesema yuko tayari kuichezea timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' endapo huduma yake itahitajika.

Mchezaji huyo ambaye amekuwa akiifuatilia Taifa Stars kwa zaidi ya miaka 11 sasa ameeleza kuwa hana kizuizi cha kujiunga na Tafa Stars lakini wenye wajibu wa kumtafuta ni Shirikisho la Soka Tanzania.

"Endapo watanitaka kuchezea Taifa Stars sina kipingamizi, mawasiliano yangu ni rahisi sana kuyapata na watayapata…sio mimi wa kuja kuomba ila wao ndio wanapaswa kuniambia unahitajika kikosini," alisema.

Pellegrino (33) anacheza nafasi ya ushambuliaji wa kushoto akichezea timu ya FK Boda ambayo inashiriki Ligi Kuu ya Norway ana urefu wa mita moja nukta tisa.

Katika kikosi cha sasa cha Taifa Stars wako wachezaji kadhaa wa Kitanzania wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi ambao wamejumuishwa. Watanzania kadhaa wamekuwa wakimtumia ujumbe mchezaji huyo kutaka arudi kujiunga na Stars.



Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Novemba 22-28, 2023 |

# Yanga yapata mfadhili Dubai



**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA soka Tanzania Bara, Yanga ya Dar es Salaam imepata mdhamini mpya kwa ajili ya michuano ya Klabu Bingwa Afrika kuanzia ngazi ya makundi.

Kampuni ya Whizpay Technology LLC ya Abu Dhabi imeamua kuidhamini Yanga kupitia kampuni yao tanzu ya Whizmo ambayo inajihusisha na huduma za kutuma fedha duniani.

Tayari mfadhili huyo ameshakaa kwenye vifua vya vya jezi za Yanga akiwa ametengeneza pia jezi ambazo ambazo mabingwa hao wametumia kama vazi rasmi la safari kuelekea Algeria0 kupambana na CR Belouizdad.

Whizmo wamechukua nafasi ya Haier ambao mwaka jana walikuwa wakikaa katika sehemu hiyo wakati wa michuano ya Kombe la Shirikisho ambapo Yanga ilifika fainali.

Uongozi wa Yanga haujasema thamani ya mkataba huo lakini hii inakamilisha kauli ya Rais wa Yanga, Mhandisi Hersi Said ambaye katika mazungumzo na Uelekeo alisema wana wadhamini wakubwa wawili ambao wanaingia kwa ajili ya kuridhishwa na mfumo wa menejimenti.

Baada ya kauli hiyo, Yanga ikaingia mkataba na Shirika la Bima la Taifa (NIC) ambalo liliamua kuweka fungu lake katika tuzo za mchezaji bora wa mwezi.

NIC wameweka kiasi cha sh milioni 900 ambazo zitakuwa zikiongezeka kila mwaka kwa mkataba wa miaka mitatu. Yanga inadhamaniwa pia na SportPesa, Haier, GSM, NIC, Azam TV, CRDB, NMB

# Taifa Stars yapoteza



IKICHEZA katika Uwanja wa nyumbani Taifa Stars imepoteza kwa mabao 2-0 mbele ya Morocco kuwania tiketi ya kucheza Kombe la Dunia.

Morocco timu namba moja bora Afrika, ilipata bao hilo pekee katika dakika ya 28 kwa mkwaju mrefu wa Hakim Ziyech ambalo lilimshibda kipa Kwesi Kawawa.


Stars walionekana kucheza kwa tahadhari na kutokutoa nafasi kwa Morocco ambao walicheza nusu fainali zilizopita za dunia.

Stars jana ilicheza ikianza na nyota wengi wa kigeni huku Kawawa akianza golini badala ya Manula aliyezoeleka lakini pia nahodha Mbwana Samatta na Simon Msuva wakiwa nje. Mbwana na Msuva waliingia kipindi cha pili lakini juhudi zao haziikuzaa matunda baada ya Morocco kuamua kuchezea kwa kujihami zaidi. Stars walijifunga bao kupitia kwa Lusajo Mwaikenda aliyekuwa akijaribu kuikoa shanvulizi lililoelekezwa mlangoni.

Wawakilishi hao wa Tanzania walilazimika kucheza pungufu kwa dakika 25baada ya Novatud Miroshi kutolewa nje.

# Fred Minziro atimuliwa kabla ya kunywa chai

**Na Mwandishi Wetu, Mbeya**



MAGEREZA wamemtimua Kocha Fred Felix 'Minziro' mapema asubuhi kabla hata muda wa chai haujafika, kutokana na matokeo yasiyoridhisha katika Ligi Kuu ya soka Tanzania Bara.

Kocha huyo alikuwa katika kuti kavu kwa muda mrefu huku ikiangaliwa kuwa ni suala la muda tu kabla ya uongozi wa timu ya Prisons kumtimua.

Minziro anakuwa Kocha wa saba kuondolewa tangu kuanza kwa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na matokeo mabaya ya vikosi walivyokuwa wakivifundisha.

Tayari Habib Kondo (Mtibwa), Zuberi Katwila (Ihefu), Robert Oliveira 'Robertinho (Simba), Cedric Kaze (Namungo) na Mwinyi Zahera (Coastal Union) wamekwishatimuliwa.

Saa moja asubuhi jana Prisons walitoa tamko la kumuondoa Minziro ambaye alikuwa na mkataba wa mwaka mmoja akiwa amesaini Mwezi Julai mwaka huu.

Katika mechi tisa, Prisons wameshinda mechi moja wakifungwa nne na kutoka sare nne huku wakishika nafasi ya 14 katika msimamo wa Ligi ikiwa imekaa mkiani kwa muda mrefu zaidi.

# Jezi za Messi kupigwa mnada

**NEW YORK,Marekani**




JEZI sita kati ya jezi zote alizovaa Lionel Messi wakati wa kampeni ya Argentina ya kushinda Kombe la Dunia zitauzwa kwa mnada.

Nahodha Messi (36), alinyanyua taji hilo baada ya timu yake kuishinda Ufaransa kwa mikwaju ya penalti katika fainali ya mwezi Desemba mwaka jana nchini Qatar.

Jezi yake kutoka katika fainali hizo imejumuishwa kwenye seti hiyo, ambayo inatarajiwa kugharimu zaidi ya pauni milioni nane katika mnada utakaoandaliwa na Sotheby's mjini New York.

Rekodi ya jezi katika soka iliyovaliwa na kuuzwa kwa gharama zaidi ni jezi ya Diego Maradona ya 'Hand of God', ambayo iliuzwa kwa £7.1m mwaka wa 2022.

Brahm Wachter, mkuu wa mapato ya kisasa ya Sotheby, alisema uuzaji wa jezi sita za Messi unasimama kama tukio kubwa katika historia ya mnada wa kisoka kuwahi kutokea.

Messi, mshindi mara nane wa Ballon d'Or, amekuwa mchezaji wa kwanza katika historia ya Kombe la Dunia kufunga katika hatua ya makundi,16 bora, robo fainali, nusu fainali na fainali ya michuano moja.